**25 JUNI, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Hamsini na Tatu – Tarehe 25 Juni, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje.

Na. 677

**Kuongeza Umri wa Vijana Kufikia Miaka 40**

**MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuongeza umri wa Vijana kufikia miaka 40 kutokana na changamoto wanazopitia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, AJIRA, KAZI NA WATU WENYE ULEMAVU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sera ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007 na Mikataba Mbalimbali ya Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia kama vile Mkataba wa Vijana wa Afrika wa Mwaka 2006 *(African Youth Chater 2006),* Sera ya Vijana ya Afrika Mashariki na Azimio la *SADC* kuhusu Maendeleo na Uwezeshwaji wa Vijana la Mwaka 2015 *(SADC Declaration on Youth Development and Empowerment)* inatambua kuwa umri wa kijana kwa Tanzania ni kati ya miaka 15 hadi 35.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na sababu hizo, Serikali kwa sasa inaona ni muhimu kuendelea na tafsiri hii ya umri kwa vijana kama inavyotambuliwa na Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Serikali nina maswali ya nyongeza; swali la kwanza kwa kuwa mwaka huu ni mwaka wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Vijiji na Vitongoji lakini pia mwakani ni Uchaguzi Mkuu wa Ubunge na Uraisi. Ni kwa nini Serikali iliamua kwamba umri wa Mtanzania kijana kupiga kura ni miaka 18, lakini hataruhusiwa kugombea mpaka afike miaka 21 Serikali ilitumia vigezo gani kuhakikisha kwamba tunafanya hivyo kwa sababu tunaamini Vyama vya Siasa vina uwezo wa ku-*train* vijana wake kuwashirikisha katika nafasi za uongozi ili wagombee?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, mwaka 2015 Bunge hili lilitunga Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa ya 2015 lakini mpaka leo ni miaka tisa sheria hii haijawahi kutekelezwa na Baraza la Vijana, haijawahi kuanzishwa. Ni kwa nini Serikali mpaka leo imeshindwa kuanzisha Baraza la Vijana la Taifa ambao kimsingi mimi naamini jukwaa hili ni muhimu kwa kuhakikisha kwamba vijana wanajadili changamoto zao pamoja na

kuhakikisha vijana wanashiriki katika mijadala mbalimbali kuwajengea uwezo kiuongozi lakini na kiuchumi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, AJIRA, KAZI NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hanje kuhusiana na umri wa kupiga kura ni miaka 18 na umri wa kugombea ni miaka 21. Tutakaa na wenzetu wa Tume ya Uchaguzi ambao wanaratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kuona ni namna gani au walifikia vipi maamuzi haya na pale ambapo tutapata majibu hayo tutaona ni namna gani tunaweka umri huu ambao unatambulika kupiga kura uwe ndiyo umri wa mtu kuweza kugombea. Kwa hiyo, tutaangalia ndani ya Serikali namna ya kufanya kwa kushirikiana na wenzetu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali lake la pili hili la Baraza la Vijana ni kweli Bunge hili lilitunga hii Sheria ya Uanzishwaji wa Baraza la Vijana. Lakini pamoja na changamoto zingine ambazo zipo ilikuwa kuna changamoto ya Sera ya Maendeleo ya Vijana yenyewe ambayo ilikuwepo ya mwaka 2007. Sasa Serikali ilianza mchakato wa ku-*review* sera ile na kuweza kuweka sera ambayo inaendana na wakati wa sasa. Mchakato ule ulianza mwaka 2022 na mchakato ule sasa uko ukingoni na muda si mrefu ile Sera ya Maendeleo ya Vijana itazinduliwa hapa nchini na baada ya sera ile kuzinduliwa basi na Baraza lenyewe la vijana sasa litafuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimtoe mashaka sasa Mheshimiwa Mbunge kwamba ile Sheria ya Baraza la Vijana tayari ipo kwa wenzetu wa *Attonery General* kwa ajili ya kufanya mapitio na kuweza kurudisha Ofisi ya Waziri Mkuu ili pale sera itapokuwa imezinduliwa, basi na Baraza lenyewe nalo litaanza.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa *Engineer* Ezra.

Na. 678

**Uhaba wa Madarasa Shule za Msingi Nemba na Nyakanazi – Biharamulo**

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Madarasa katika Shule za Msingi Nemba na Nyakanazi ambazo zina Wanafunzi wengi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa ujenzi wa madarasa katika shule mbalimbali za msingi kufuatia ongezeko la wanafunzi. Katika kutatua changamoto ya upungufu wa madarasa kwenye maeneo hayo shule shikizi tatu za msingi (Nemba B, Chakirabu na Kikaimara) zilianzishwa na sasa zimesajiliwa kuwa shule kamili.

Mheshiwa Naibu Spika, mwaka 2023/2024, Serikali ilijenga shule mpya ya Ilagaza katika eneo la Nyakanazi iliyogharimu shilingi milioni 400. Aidha, Serikali ilijenga Shule ya Msingi Kizota kwa gharama ya shilingi milioni 250. Vilevile, kupitia Mradi wa *BOOST* Serikali imejenga vyumba vinne (04) vya madarasa katika Shule ya Msingi Nyakanazi ili kuiongezea nafasi shule hiyo kwa lengo la kupunguza msongamano wa wanafunzi.

**NAIBU SPIKA:** *Engineer* Ezra.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Ahsante sana, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na nishukuru kwa ajili ya ujenzi wa hizi shule ambazo Mheshimiwa Waziri amezitaja na bado nyingine za sekondari zimepatikana pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tukiangalia rekodi ya Sensa ya Mwaka 2022 Jimbo la Biharamulo ndiyo linayoongoza kwa idadi ya watu kwa Mkoa wa Kagera *that means* tuna watoto wengi sana ambao bado wanahitaji huduma. Kwa hiyo, ni nini mpango wa Serikali kwenye kutuletea vyumba vya madarasa vingine kwa ajili ya maeneo mengine ambayo bado yana watoto wengi wasiyoipata hiyo huduma kwa Shule za Msingi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia watoto hawa wanapofaulu kwenda Sekondari kwa sababu ni wengi bado wana uhaba wa vyumba vya madarasa na pia wanapoelekea Sekondari. Kwa sababu ni Wizara hii hii na ni jambo hili la vyumba vya madarasa naomba kusikia pia kauli ya Serikali juu ya watoto wanaofaulu kwenda Sekondari Wilaya ya Biharamulo waweze kuongezewa vyumba vya madarasa ili wapate *accommodation* nzuri wanapoenda sekondari. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa na nzuri ya uwakilishi anayoifanya. Lakini kuhusiana na swali lake la kwanza napenda nianze kukumbushia msingi mzima wa ugatuzi wa madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi ni kuhakikisha kwamba Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa zinakuwa na *fees code centralization,* yaani zinaweza zenyewe kujitegemea kwa maana kutafuta mapato na kuweza kuendeleza miundombinu ya msingi. Kwa sababu jukumu la msingi la kutengeneza miundombinu mbalimbali liko kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Lakini tunamshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Miradi ya *BOOST* kwa ajili ya Shule za Misingi na Mradi *SEQUIP* ameleta fedha nyingi sana kwa ajili ya kuunga mkono jitihada za Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa na ndiyo maana kila mwaka Serikali imekuwa ikituma fedha katika huu Mradi wa *BOOST* kwa

ajili ya kwenda kuongeza madarasa katika shule zetu za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika muktadha wa swali lake yeye kwa maana ya Shule za Sekondari. Sasa kwenye swali lake la pili katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 kupitia Mradi wa *SEQUIP* Serikali imeleta jumla ya shilingi milioni 584.2 kwa ajili ya Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Lusahunga, lakini pia imeleta jumla ya shilingi milioni 100 kwa ajili ya nyumba za walimu. Kwa hiyo, Serikali imekuwa ikileta fedha kila mwaka wa fedha kuhakikisha kwamba inaongeza nguvu pale ambapo Mamlaka za Serikali za Mitaa tayari zimeanza na zenyewe kuunga mkono au kujenga miundombinu hii muhimu katika Sekta ya Elimu. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali itaendelea kuhakikisha inaboresha miundombinu ya Sekta ya Eilimu na pia kwenye Jimbo lako Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Maryam Azan.

Na. 679

**Vifaa Tiba katika Majengo ya Hospitali**

**MHE MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaweka vifaa tiba katika majengo ya huduma za mama na mtoto kwenye halmashauri mbalimbali nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali za halmashauri. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 hadi 2023/2024, jumla ya shilingi bilioni 186.3

zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba vikiwemo vifaa vya huduma ya mama na mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025, Serikali imetenga shilingi bilioni 66.7 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba ambapo kipaumbele kimewekwa kwenye vifaa tiba vya huduma za mama na mtoto kwenye vituo vyenye upungufu mkubwa zaidi kote nchini. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maryam.

**MHE MARYAM AZAN. MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa bado kuna baadhi ya hospitali wakinamama wanapokwenda kujifungua huwa wanaambiwa watoe hela kwa ajili ya vifaa je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili vifaa bila watumishi bado kazi bure, upi mpango wa Serikali kuhusu kutoa ajira kwa watumishi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ni kweli kwamba kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya vituo vya huduma za afya kote nchini kutoza gharama za vifaa na hasa *grooves* na vifaa vingine kwa wajawazito wanapofika kupita huduma za afya ya mama na mtoto. Serikali kupitia Sera Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais, TAMISEMI tulikwisha elekeza kwamba huduma kwa kinamama wajawazito zinazohusiana na masuala ya kujifungua na watoto wenye umri chini ya miaka mitano zinatolewa bila malipo yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kauli ya Serikali naomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuwasisitiza Wakurugenzi wa Halmashauri kote nchini, Waganga Wakuu wa Halmashauri na Waganga Wafawidhi

kuhakikisha wanasimamia maelekezo ya Sera, lakini pia wanasimamia maelekezo Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kuwa na Vifaa Tiba vyote vinavyohitajika kwa ajili ya kinamama wajawazito na watoto wa chini ya miaka mitano ili huduma hizo zitolewe bila malipo yoyote kama ilivyo maelekezo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuajiri Watumishi wa Sekta ya Afya wa kada mbalimbali na kuwapeleka kwenye Vituo vya Afya vyote vya huduma ya afya msingi. Katika kipindi cha miaka mitatu zaidi ya watumishi 18,876 wameajiriwa na hivi karibuni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora alishatangaza kutolewa kwa kibali cha watumishi wengine wa afya karibu elfu kumi. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba mara ajira hizo zikitangazwa tutahakikisha watumishi wanapelekwa kwenye vituo vyetu vyote. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Asia.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je ni lini Serikali itaweka vifaa tiba katika majengo ya mama na mtoto katika Kituo cha Afya Endasak pamoja na Gisambalang Jimbo la Hanang? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Vituo vya Afya vya Endasak na Gisambalang ni vituo ambavyo Serikali ilipeleka fedha, vituo hivyo vimejengwa vimekamilika vimeanza kutoa huduma za awali. Lakini Mheshimiwa Rais alishapeleka fedha za Vifaa Tiba katika Halmashauri zote 184, tunatambua kwamba Vifaa Tiba vile bado havitoshelezi ikiwemo katika vituo hivi vya Endasak na Gisambalang. Nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwenye bajeti ya mwaka ujao wa fedha Serikali imetenga zaidi ya

bilioni 66.7 ya vifaa tiba na tutahakikisha tunatoa kipaumbele katika vituo hivi vya afya, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Shamsia Azizi, Unatakiwa useme kwa niaba siyo mimi nikuulize, sema wewe.

Na. 680

**Kukamilisha Ujenzi wa Kituo cha Afya Mkunwa - Mtwara Vijijini**

**MHE. STELLA S. FIYAO K.n.y. MHE. SHAMSIA A. MTAMBA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha Ujenzi wa Kituo cha Afya Mkunwa - Mtwara Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Mkunwa kilianza ujenzi mwaka 2019/2020 ambapo ujenzi wake ulianza kwa ramani ya majengo ya hospitali. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 1.5 zimeishatolewa kwa ajili ya ujenzi wa majengo saba (7); jengo la OPD, jengo la wazazi, jengo la dawa, jengo la maabara, jengo la mionzi, nyumba ya mtumishi na kichomea taka. Majengo haya yapo kwenye hatua mbalimbali za ujenzi na ili kukamilika, kiasi cha shilingi milioni 900 kinahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo hayo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza; swali la kwanza, Mheshimiwa Waziri Mkuu

alipofanya ziara katika Jimbo la Mtwara Vijijini aliagiza kwamba fedha zitolewe ili kituo hiki cha afya kiweze kukamilika sasa nakata kujua ni lini fedha itapelekwa kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyotoa agizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali langu la pili nataka kujua ni lini sasa mtafanya ukamilishaji katika Kituo cha Afya Ndola na Itale ili wananchi waweze kupata huduma? Kilichopo Wilaya ya Ileje? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ni kweli kwamba Serikali ilishapeleka fedha bilioni 1.5 kwa ajili ya kukamilisha Kituo cha Afya hiki cha Mkunwa na tunafahamu kuna majengo kadhaa ambayo bado hayajakamilika na Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya Ziara katika Jimbo la Mtwara vijijini alitoa maelekezo na sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kazi yetu ni kutekeleza maelekezo ya viongozi wetu wa kitaifa. Kwa hivyo, nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumeishaweka kwenye mpango wa bajeti wa mwaka ujao 2024/2025 na tutapeleka fedha hizo kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu ambayo imesalia na kuhakikisha inaendelea kutoa huduma bora kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, kuhusiana na vituo hivyo vya afya viwili katika Halmashauri ya Ileje ambavyo umevitaja Serikali ilishaweka mpango; kwanza, tuliainisha maeneo yote ya kimkakati ya kujenga vituo vya afya, lakini tumeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kwenda kujenga vituo na kumalizia. Kwa hiyo, nikuhakikishie tu kwamba viko kwenye mpango na tutahakikisha fedha inapopatikana tunapeleka kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vituo hivyo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilango.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, Wabunge wote wa Majimbo tuliulizwa kila mmoja

achague kata ambayo atajengewa Kituo cha Afya cha Kimkakati. Baada ya kufanya hivyo tulipewa fomu kabisa tukajaza, tukarudisha Serikalini na tukarudi kwa wananchi tukawaambia kwamba Serikali inajenga Kituo cha Afya cha Mkakati. Je, Serikali, mtuambie, maana yake wananchi tuliwaambia, hivi vituo vya afya kila Jimbo vya Kimkakati vitajengwa lini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ni kweli dhamira njema ya Serikali yetu ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kusogeza huduma ya afya karibu zaidi na wananchi na ndiyo maana kazi ya Ujenzi wa Vituo vya Afya katika Kata za Kimkakati imeendelea na kwa kipindi cha miaka mitatu zaidi ya Vituo vya Afya 878 vimejengwa katika Kata zetu kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba kila Jimbo linapata kituo cha afya kimoja na tulishaleta orodha hapa kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema, nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba orodha ile tunayo, tunafahamu Kata za kimkakati na tayari Serikali ina-*mobilize* fedha kwa ajili ya kwenda kuanza ujenzi wa vituo hivyo. Kwa hiyo, niwatoe mashaka Waheshimiwa Wabunge Serikali iko kazini na tutahakisha fedha ikipatikana tunakwenda kujenga Vituo vya Afya katika maeneo yaliyoainishwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Francis.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Viongozi akiwemo Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi amewaahidi Wananchi wa Kinyangili kwamba atakarabati kile Kituo cha Afya kifanane na vingine. Ni lini Serikali itatimiza ahadi hii ya Viongozi Wakubwa wa Chama? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, hoja hii Mheshimiwa Mbunge ameifuatilia mara kadhaa na tayari Ofisi ya Rais, TAMISEMI tulishaingiza kwenye Mpango wa vituo ambavyo viko kwenye mpango wa kwenda kuvikarabati lakini pia kuviongezea miundombinu ambayo inapungua. Kwa sasa tumeweka kipaumbele kwenye kukamilisha hospitali chakavu za halmashauri na baada ya hapo tutakwenda kwenye vile vituo vya afya vyote 202 kikiwemo kituo cha afya hicho katika Halmashauri ya Mkalama. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mulugo.

**MHE. PHILIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, Wilaya ya Songwe ni pana na *very scattered* na Wananchi wa Kata za Kanga na Namkukwe wamejitahidi kwa nguvu zao kujenga Vituo vya Afya na tayari maboma yapo, lini Serikali italeta vifaa kumalizia vituo hivyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nawapongeza wananchi wa Kata hizo za Namkukwe na Mkanga ambazo amezitaja Mheshimiwa Mbunge katika Halmashauri ya Songwe. Nawapongeza sana kwa kweli, kwa kuchangia nguvu zao kuanza ujenzi wa vituo hivyo vya afya, huo ndio mpango wa maendeleo ya afya ya msingi, wananchi wanaanza Serikali inafanya umaliziaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, vituo vyote ambavyo vipo kwenye kata za kimkakati ambavyo tumeshaainisha vinakidhi vigezo, tunakwenda kuvitengea fedha, kwa ajili ya umaliziaji. Kwa hiyo, vituo hivyo pia, tutavipa kipaumbele wakati wa umaliziaji wa vituo vingine vya afya. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

Mheshimiwa Minza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kata ya Sangamwalugesha ni kata kubwa sana, ina wakazi 10,500 lakini haina kituo cha afya. Je, ni lini sasa Serikali itajenga kituo cha afya katika kata hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo Kata ya Sangamwalugesha ambayo ina idadi kubwa ya wananchi, pia, ina umbali mkubwa kutoka kituo cha afya cha karibu zaidi. Ni miongoni mwa kata ambazo Mkoa wa Simiyu uliwasilisha Ofisi ya Rais - TAMISEMI na tulishamuelekeza pia, Mkurugenzi wa Halmashauri kuanza kutenga fedha kupitia mapato ya ndani, wakati Serikali Kuu inatafuta fedha, kwa ajili ya kwenda kumalizia majengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, natumia nafasi hii kusisitiza kwamba, Mkurudenzi wa Halmashauri ahakikishe anatenga fedha, kwa jili ya kuanza ujenzi. Pia, nawakumbusha Wakurugenzi wa Halmashauri kote nchini kwamba, ni wajibu wao maeneo yale ambayo ni vipaumbele, kutenga fedha za mapato ya ndani katika ile 40% mpaka 70%, ili ujenzi uanze wakati Serikali Kuu inatafuta fedha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri ulienda kwenye Kijiji cha Tiling'ati ukaona Zahanati ya Tiling'ati na ukawaambia wamalize kupaua wewe utaenda kufanya *finishing*. Ni lini utaenda pale kumalizia hiyo *finishing* uliyowaahidi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kweli tulifanya ziara na Mheshimiwa Getere katika Jimbo lake la Bunda Vijijini na tulienda kwenye Zahanati ya Tiling'ati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nawapongeza Wananchi wa Kijiji cha Tiling'ati kwa kazi nzuri na kubwa ambayo waliifanya kwa kuchanga michango yao na kuanza ujenzi na Mheshimiwa Mbunge amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na ahadi ya milioni 20, kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati ile. Tayari tumeweka kwenye mpango na, Mheshimiwa Getere, fedha ikipatikana mara moja tutapeleka, kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati hiyo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Tunaendelea. Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Aida, kwa niaba, Mheshimiwa Deus Sangu.

Na. 681

**Changamoto ya Umeme Wilayani Nkansi**

**MHE. DEUS C. SANGU K.n.y. MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza changamoto ya umeme Wilayani Nkasi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya umeme Wilayani Nkasi inatokana na Mkoa wa Rukwa, ikiwemo Wilaya ya Nkansi, kutokuwa kwenye Grid ya Taifa ambapo mara nyingi inapata umeme mdogo ukilinganisha na mahitaji. Ili kuondokana na changamoto hiyo, Serikali kupitia *TANESCO* inatekeleza mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 400 wa *Tanzania – Zambia Interconnector (TAZA)* kutoka Iringa mpaka Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu utaunganisha Mkoa wa Rukwa, ikiwemo Wilaya ya Nkansi, na Gridi ya Taifa na hivyo kuwezesha upatikanaji wa umeme wa kutosha kutoka kwenye Gridi. Aidha, kitajengwa kituo cha Kupoza Umeme cha Nkasi, ambacho kitasaidia kupoza umeme unaotoka Sumbawanga pamoja na kuweka *feeder* tatu za kulisha umeme Wilayani Nkasi. *Feeder* hizi zitasaidia ufuatiliaji hasa kunapokua na tatizo la umeme ukilinganisha na hali ilivyo sasa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sangu.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya bei, hasa katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Namanyele na Laela, ziliathiriwa ambapo kutoka shilingi 27,000 mpaka shilingi 320,000 kutokana na Sheria ya Mipango Miji, lakini kiuhalisia Sura ya Mamlaka ya Miji hii midogo ni ya vijiji. Je, Serikali mna mpango gani wa kushusha bei kurudi kuwa, shilingi 27,000 ili kuwapa nafuu Wananchi wa Mamlaka ya Miji hii kuunganisha umeme?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Mkandarasi anayetekeleza mradi wa umeme Mkoa wa Rukwa, hasa Jimbo la Kwela, *speed* yake ni ya kusuasua, hasa katika Kata ya Mnokola, Kilangawala na Milepa. Nataka kupata kauli ya Serikali, ni lini mtamsimamia mkandarasi huyu kikamilifu, ili aweze kutekeleza majukumu kwa sababu, tumelalamika mara nyingi hapa Bungeni? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na maeneo ambayo wana-*charge* shilingi 320,000 badala ya shilingi 27,000 katika maeneo ya Namanyele na eneo lingine ambalo Mheshimiwa Mbunge amesema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, tumefanya mapitio ya maeneo ambayo tuliona hayastahili kuwekewa kiasi cha shilingi 320,000 na tumeshauri, ili iweze kushuka mpaka shilingi 27,000. Katika maeneo haya tumeshapitia maeneo 1,500 na tumejiridhisha kwamba, inabidi yaende kwenye shilingi 27,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na maeneo haya mawili ambayo Mheshimiwa Mbunge amesema tutaenda kupitia kuona kama yapo katika yale maeneo ambayo tumesema, inabidi yatoke shilingi 320,000 mpaka shilingi 27,000. Kama yapo hapo tutaendelea na utekelezaji kwa kadiri muda unavyoenda na upatikanaji wa fedha, lakini kama hayapo, basi tutajiridhisha kuona kama maeneo haya yanatakiwa kushushwa mpaka shilingi 27,000 na baada ya hapo tutayaingiza katika mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na haya maeneo ya Kwela, Mnokola, Kiwangawala na hilo lingine ambalo amesema Mheshimiwa Mbunge; kwa kweli, ni kweli huu Mradi wa Tanzania – Zambia *Interconnector* ulikuwa unasuasua kidogo kwenye baadhi ya maeneo. Mapema mwaka huu Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati walifanya ziara kwenye mradi huu na kukwamua yale matatizo ambayo yalikuwa yanasababisha mradi kutoenda kwa kasi ambayo sisi tumetarajia. Nakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati wameshafanyia kazi na tutaendelea kumsimamia mkandarasi, ili aweze kutekeleza vizuri mradi huu uweze kukamilika kwa wakati. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza, naishukuru Serikali kwa kupeleka Miradi ya Umeme wa *REA* kwenye Wilaya ya Tanganyika. Kwenye Wilaya ya Tanganyika mmepeleka Umeme wa *REA* kwenye Kata ya Mwese ambao umewafikia wananchi. Kwa bahati mbaya sana zile taasisi muhimu kama soko, Parokia na eneo la Msikiti na shule ya sekondari na msingi hakujapelekwa umeme. Ni lini mtapeleka huduma hiyo iwafikie wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Kakoso, Mbunge wa Tanganyika. Ni kweli katika maeneo mengi, ikiwemo hii Mwese, kuna baadhi ya taasisi hazijafikiwa, lakini tumeshatoa maelekezo kwa yale maeneo ambayo hayadizi mita 500, basi wafanyie kazi kuona taasisi ambazo zipo kwenye ukubwa wa sehemu ambapo umeme ulipo mpaka mita 500 yaweze kuunganishwa na umeme kwa sababu, wote tunafahamu umuhimu wa taasisi hizi katika mendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, katika Kata hii ya Mwese ambapo Mheshimiwa amesema maeneo ya parokia, msikiti, shule za msingi na sekondari tutafanyia kazi. Tutakwenda, ili kuweza kuona kama maeneo haya yapo kwenye ukubwa huo na kuweza kupatiwa umeme, lakini kama maeneo haya yapo mbali tutaangalia kuona kwenye mradi wa vitongoji kuona namna gani maeneo haya yanafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, ni azma na nia yetu ya dhati kuhakikisha maeneo yenye taasisi zote za muhimu yanafikiwa na umeme kwa sababu, Serikali inawekeza fedha nyingi sana, hususan kwenye shule za msingi na sekondari. Na dhamira yetu ni kuhakikisha maeneo haya yenye taasisi zinazoleta huduma kwa jamii na zenyewe zinaweza kupata umeme, ili tuweze kuboresha zaidi mazingira ya kujifunza na kujifunzia kwenye shule za msingi na sekondari. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kikoyo.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Utekelezaji wa Miradi ya *REA* katika Wilaya ya Muleba unasuasua. Serikali ina kauli gani kumuhimiza mkandarasi amalize ile kandarasi aliyopewa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na pia, nashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Kikoyo. Nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kweli, ni mkakati wetu kuhakikisha miradi hii inakamilika kwa wakati. Namhakikishia nitafanya ziara katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge, ili kujionea na kuendelea kumsisitiza mkandarasi aweze kuongeza kasi hii ya kupeleka umeme kwenye vijiji ambavyo vimebakia, ili iweze kufanyika kwa haraka wananchi waweze kupata umeme. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Fedha. Mheshimiwa Sichalwe.

Na. 682

**Kuboresha Mpaka Kati ya Zambia na Tanzania Kudhibiti Utoroshwaji wa Bidhaa**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaboresha Mpaka kati ya Zambia na Tanzania, ili kudhibiti njia za panya ambazo mazao na bidhaa nyingine hutoroshwa bila kulipiwa kodi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** aljibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, katika kudhibiti utoroshwaji wa mazao na bidhaa katika mipaka ya Tanzania na Zambia, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* na Mamlaka ya Mapato Zambia *(ZRA)* ziliingia makubaliano yanayoelekeza hatua mbalimbali za kuchukua kwa kila nchi. Utekelezaji wa hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Mfumo wa Uondoshaji Mizigo wa *TANCIS* umeunganishwa na Mfumo wa *ASYCUDA World* wa Zambia, ili kubadilishana taarifa na kurahisisha taratibu za uondoshaji mizigo;

(ii) Serikali imesimika midaki za kukagua mizigo inayobebwa na abiria pamoja na magari;

(iii) Serikali ya Zambia kupanua barabara na eneo la maegesho ya upande wa Nakonde, ili kupunguza msongamano upande wa Tunduma; na

(iv) Kuendelea kubainisha vihatarishi vilivyopo katika magari ya mizigo yanayopita Mpaka wa Tanzania na Zambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja hatua hizo, Serikali kupitia *TRA* inaendelea kuimarisha doria, kwa ajili ya kudhibiti maeneo yote ya mpaka wa Tanzania na Zambia kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama, ili kulinda mapato ya Serikali. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuendelea pale nilipoishia kwenye mchango wangu wa jana kwamba, kulingana na jiografia ya nchi yetu kupakana na Nchi ya Kenya kuna mageti *(stop border post)* Namanga, Tarakea na Holili. Je, kama sisi tunapakana na Nchi ya Zambia, upi ni mkakati wa Serikali kuona namna ya kuongeza mageti, ili utoroshaji huu usiendelee? Tuna Geti moja la Tunduma, liongezeke Geti la Chipumpu, Kapele pamoja na Geti la Kasesha, Kalambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa, mchango huu kwa kuongeza geti, ili kuzuia utoroshaji wa mazao na bidhaa nyingine ambazo zinaingia nchini kinyume na utaratib nimekuwa nikichangia kuanzia Mwaka 2021. Natamani Serikali itueleze je, mmeshawasiliana na wenzetu wa Zambia kuwapa wazo hili na wao kuona kama ni fursa tunaweza tukaitumia kuongeza chanzo cha mapato? Kama ndio, Zambia wanasemaje? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza. Serikali kupitia *TRA* inafanya *survey* kwenye milango yote ya mipaka kwa Nchi yetu ya Tanzania na nchi nyingine za jirani. Kwa hiyo, Serikali itakapofika hatua imejiridhisha, basi tunaweza tukachukua hatua ya kujenga au kuongeza geti kutoka moja yakawa mawili na hadi kufikia matatu, ikionekana ipo tija ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Serikali ya Tanzania pamoja na Serikali ya Zambia kupitia *TRA* na *ZRA* tunafanya mawasiliano ya kila siku, ili kuona tunaboreshaje kuzuia bidhaa hizi zisipite kwa njia za panya au za magendo, ili kuongeza mapato kwa nchi yetu. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi. Mheshimiwa Pathan.

Na. 683

**Fidia kwa Wananchi Wanaopisha Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege – Nachingwea**

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawalipa fidia Wananchi waliopisha upanuzi wa Uwanja wa Ndege Nachingwea?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI K.n.y. WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea na jitihada mbalimbali katika kuhakikisha suala la ulipaji fidia kwa wananchi wanaopisha upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Nachingwea linakamilika. Aidha, hatua ya awali ya kutambua wafidiwa na mali zao imekamilika uwandani na tayari maombi ya fedha hizo

za fidia yamewasilishwa Wizara ya Fedha, kwa ajili ya ulipaji. Vilevile, Serikali itahakikisha kuwa, wananchi wote wanaopisha maeneo yao, kwa ajili ya upanuzi wa Kiwanja hicho wanalipwa fidia zao stahiki. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pathan.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu ya Serikali. Naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni zaidi ya miaka saba au nane Wilaya ya Kilwa imepisha upanuzi wa uwanja wa ndege na zaidi ya miaka sita kwa Wilaya ya Nachingwea wananchi wamepisha upanuzi wa uwanja wa ndege. Serikali inasema Sheria inasema wananchi wanatakiwa walipwe si zaidi ya miezi sita. Je, kukaa kwa muda mrefu huko bila kuwalipa hao wananchi Serikali haioni kwamba, inazidi kuwadididimiza hao wananchi kimaendeleo? Swali la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Naomba kauli thabiti ya Serikali. Je, ni lini malipo ya wananchi waliopisha Uwanja wa Ndege wa Kilwa na Nanchingwea watapata stahiki zao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI K.n.y. WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tathmini ilifanyika kipindi hicho alichokisema, lakini ndio maana sasa hivi imefanywa tathmini upya, ili kupata thamani ya sasa. Nimhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kuhakikisha kwamba, inajenga hivi viwanja. Ninavyoongea hivi sasa ni kwamba, hiki Kiwanja cha Kilwa Kivinje pamoja na Nachingwea tayari majedwali yake yapo Hazina. Tunachosubiri ni Hazina iweze kutoa fedha, ili tuweze kuwalipa wananchi hao kwa thamani ya sasa. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Dkt. Kimei.

Na. 684

**Fidia kwa Wananchi wa Kahe/Chekereni – Njiapanda**

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawalipa fidia Wananchi wa Kahe/Chekereni na Njiapanda ambao maeneo yao yalichukuliwa na *TANROADS* Mwaka 2013? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uthamini wa Mali za Wananchi wa Kahe/Chekereni – Njiapanda (Himo) watakaoathiriwa na mradi huo ulifanyika Mwaka 2013. Hata hivyo, kutokana na muda mrefu kupita bila kulipa fidia hiyo, Serikali imerudia zoezi la uthamini na taarifa ya uthamini imeidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali Tarehe 8 Machi, 2024. Kwa sasa, Serikali inaendelea kutafuta fedha, kwa ajili ya kulipa fidia kwa mali za wananchi watakaoathiriwa na mradi huo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Dkt. Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akanihakikishia kwamba, kwa vile tathmini imefanyika baada ya miaka 10 ya madai haya. Je, ndani ya miezi sita hii Serikali ipo tayari kulipa haya madeni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kwamba, Wananchi wa Mabungu pale Uchira na wenyewe wanadai kwa kipindi hicho hicho cha miaka 10 na wao pia walifanyiwa tathmini. Je, unaweza ukanihakikishia kwamba, na wao watalipwa ndani ya miezi hii sita? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba nijibu maswali yote mawili ya Mheshimiwa Kimei, Mbunge wa Vunjo, kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Machi tumefanya tathmini upya na kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, tathmini hiyo imeshaidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali. Kwa maana hiyo ni kwamba, Serikali ina nia ya dhati kabisa kuhakikisha kwamba, ndani ya kipindi kifupi wananchi hawa wawe wamelipwa. Sisi kama Wizara ndio maana tumeshakamilisha kazi yote. Kwa hiyo, tunachosubiri sasa hivi ni wenzetu wa Hazina waweze kutoa fedha, ili wananchi hao waweze kulipwa katika kipindi ambacho Mheshimiwa Mbunge amekihitaji. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Barabara ya kutoka Handeni hadi Mafleta (kilometa 20) ni takribani mwaka wa pili sasa, lakini wananchi waliopisha barabara hii hawajalipwa fidia. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini wananchi hawa watalipwa fidia?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, wananchi wale walishafanyiwa tathmini na sisi kama Wizara tulishawasilisha ile tathmini, kwa maana ya thamani ya fidia yao, kwa ajili ya kulipwa. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, wananchi wawe na Subira, Serikali ipo inajipanga kuhakikisha kwamba, wanalipwa hiyo fidia yao. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Barabara ya Njombe – Makete, wananchi wa Eneo la Ramadhan na Tandala mpaka leo hawajalipwa fidia na barabara imejengwa zaidi ya miaka sita. Ni lini wananchi hao watalipwa fidia yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba Mheshimiwa Deo Mwanyika, kama ni miaka sita wananchi wote hawajalipwa, hilo litakuwa ni *special case*. Kama walishaondolewa na hawajalipwa naomba tuweze kukaa naye, ili tuone changamoto ni nini, halafu nadhani nitatoa majawabu sahihi kwa Mheshimiwa Mbunge. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saputu.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Barabara ya Mianzini kuja Lumulingiringa – Kimnya mpaka Ngara Mtoni – Levolosi, baadhi ya wananchi hawakulipwa fidia. Je, ni lini Serikali itakamilisha fidia hiyo kwa wananchi wale wanaotakiwa kupisha barabara hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ni kweli barabara anayoisema, yapo maeneo ambayo hapakuwa na barabara kabisa na Serikali inachofanya ni kujiridhisha na kuona kwamba, kule ambako barabara itapita, wananchi wale ndio watakaolipwa. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, anafahamu kuna watu wapo uwandani na kazi ikishakamilika na taarifa zikakaa sawa, basi wananchi hao watalipwa kwa sababu barabata hiyo tunaihitaji haraka sana. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kurudia tathmini ya fidia kwa wananchi waliopisha Barabara ya

Mbasa kuelekea Malinyi imeshafanyika na ni zaidi ya miaka minne sasa wananchi wanasubiri fidia hiyo. Je, ni lini wataanza kulipwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kama tathmini ilifanyika miaka minne na hawajalipwa, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge hatutalipa kwa thamani hiyo. Tutalazimika kurudi tena kufanya tathmini upya ili tuweze kupata thamani ya sasa na ndiyo wananchi hao waweze kulipwa kwa gharama ya sasa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Turky; kwa niaba Mheshimiwa Ramadhan.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ni Mheshimiwa Ramadhan kwa niaba ya Mheshimiwa Toufiq Salim Turky, Mbunge Mpendae.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, ninaomba swali lake namba...

**NAIBU SPIKA:** Hebu, hebu rudia tena; unajiita mwenyewe Mheshimiwa? Mheshimiwa tunakuita sisi, wewe hujiiti Mheshimiwa. *(Makofi/Kicheko)*

Haya endelea.

Na. 685

**Viwanda vya Kuchinja, Kuchana na Kusindika Mifugo Nchini**

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN K.n.y. MHE. TOUFIQ SALIM TURKY** aliuliza: -

Je, upi mpango wa kuhakikisha viwanda vya kuchinja, kuchana na kusindika nyama vinavyokidhi vigezo vya kusafirisha nje ya nchi vinajengwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kuweka mazingira wezeshi ili kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya kuchinja, kuchakata na kusindika mifugo na mazao yake vinavyokidhi vigezo vya kusafirisha nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na kuhamasisha uanzishaji wa viwanda kupitia eneo maalumu la uwekezaji *(EPZ)* kwa ajili ya soko la nje ya nchi ambapo wawekezaji wanapata msamaha wa kodi ya mapato, kodi ya mitambo na vifaa vya kuchakata na kusindika nyama. Pia, Serikali imeondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kwenye vifaa vya kuchakata nyama kwa wadau wanaoomba msamaha huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na jitihada hizi za Serikali, viwanda vyenye viwango na ithibati ya kimataifa ya kusafirisha nyama nje ya nchi vimeongezeka kutoka viwanda viwili mwaka 2018/2019 hadi kufikia viwanda sita mwaka 2023/2024.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ramadhan.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, *trending* inaonesha kwa sasa hoteli, Zanzibar pamoja na Arusha wanaagiza nyama kutoka nje ya nchi, *South Africa, Argentina* na nchi nyingine. Ni lini Serikali itaweka jitihada za kuhakikisha nyama ya kwetu Tanzania inatumika kwenye maeneo hayo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa anachosema Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna baadhi ya hoteli ambazo ziko ndani ya nchi zinaagiza nyama kutoka nje ya nchi na hii siyo kwa sababu hatuna viwanda vya Kimataifa. Tuna viwanda vizuri sana vya nyama ndani ya nchi yetu ambavyo vinakidhi vigezo vya Kimataifa na viwanda hivyo vimekuwa vikifanya vizuri ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto tuliyonayo sisi na hili lazima tuambizane ukweli kwamba nyama yetu sisi haina ubora wa kufika nje ya nchi na kupata soko la Kimataifa. Hii ni kwa sababu, sisi tunachokijua ni mfugo kuzaliwa na mfugo kuchinjwa lakini hapa katikati hatufuatilii maendeleo ya mfugo wala hatujui historia yoyote ya mfugo, ikiwa ni pamoja na matibabu ya mfugo. Mfugo huyu anaoga nini hatujui, mfugo anakula nini hatujui, anakunywa tope au maji hatujui, ana chanjo hajachanjwa hatujui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wenzetu kule nje wanafuatilia hivi vyote na ndiyo maana wanakuwa na kigezo cha kupata soko la Kimataifa. Sasa, nini mkakati wa Serikali? Serikali ndiyo maana tumekuja na mpango wa mwaka huu, lazima mifugo yetu tuichanje kwa lazima nchi nzima ili iweze kupata soko la Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumwombe Mheshimiwa Mbunge pamoja na wadau wengine wa sekta hii ya mifugo kushirikiana kwa pamoja kuhakikisha kwamba mwaka huu tunaanza zoezi hili la kuchanja mifugo yetu na tupunguze siasa kwenye zoezi hili ili liweze kufanikiwa. Maana yake tumekuwa tukianzisha mipango hii, huko mbele inaingia siasa, mipango inakwama, shughuli zinasitishwa na mambo mengine yanazidi kuharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ili tuweze kupata soko la ndani ya nchi na nje ya nchi ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** ...lazima tufuate utaratibu wote wa kutibu mifugo yetu ili tuweze kupata soko la ndani ya nchi na nje ya nchi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Francis Ndulane.

Na. 686

**Hitaji la Malambo Kata za Miguruwe, Samanga, Tingi, Njinjo na Mitole - Kilwa Kaskazini**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga malambo ya kuhifadhia maji ya kunyweshea mifugo katika Kata za Miguruwe, Samanga, Tingi, Njinjo na Mitole?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuwekeza katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji ya mifugo ili kutatua changamoto kubwa iliyopo ya upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali za kujenga malambo na kuchimba visima virefu kwa ajili ya maji ya mifugo, bado mahitaji ya miundombinu ya maji kwa mifugo ni makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya upatikanaji wa maji ya mifugo katika Kata ya Miguruwe, Samanga, Tingi, Njinjo na Mitole katika Jimbo la Kilwa Kaskazini na imeshaweka maombi haya kwenye vipaumbele vya Wizara ili yajumuishwe katika mpango wa Bajeti ya Wizara ya mwaka

2025/2026 kulingana na upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha huduma ya malisho katika Wilaya za Kilwa, Nachingwea na Liwale Mkoani Lindi ili kutatua changamoto ya migogoro ya wakulima na wafugaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ningependa kujua, kwa kuwa Serikali haijawahi kuitisha kongamano lolote la Kitaifa kwa kuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge katika kutatua changamoto ya wakulima na wafugaji. Je, ni lini itaitisha kongamano hili ili tuweze kutatua changamoto hii ambayo inakabili Taifa kwa sasa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali kwa sasa kuhusiana na kuongeza malisho nchini tayari tumekwishatangaza na siku ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ninadhani mlimwona Mheshimiwa Waziri. Alikuja na mbegu ambazo ziko tayari kusambazwa kwa nchi nzima kwa ajili ya kuwagawia wafugaji waweze kuzalisha mbegu kwa ajili ya mifugo yetu katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mbegu hizo ziko tayari. Huo ndiyo mkakati namba moja, kuongeza malisha ambayo yatasaidia wafugaji wetu katika maeneo hayo. Tuna aina nyingi sana za mbegu zaidi ya aina tano ambazo mfugaji akizipanda zina uwezo wa kujiotesha na kuzaliana na kuzaliana katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuko tayari kupeleka kwenye jimbo lako Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo

tumeshaanza kupeleka katika maeneo mengine ya nchi hii, mbegu za malisho ambazo zitatusaidia kupunguza sana kelele hizi za wafugaji na wakulima katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili la kongamano, Mheshimiwa Mbunge tumelichukua tutakwenda kulifanyia maandalizi na mara litakapokamilika tutawaletea taarifa ili tuweze kupata elimu ya pamoja, wataalamu watatupatia elimu ya pamoja sisi Wabunge ili tuweze kupata ...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Amar. *(Makofi)*

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante; kwa kuwa mtu ni afya lakini pia hata mifugo inahitaji afya bora ikiwa ni pamoja na kuoga, chanjo na matibabu. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga majosho ili ng'ombe wetu nao waweze kuoga na kuwa na afya njema, kwenye Kata ya Shabaka, Mwingiro, Kaboha, Izunya yakafika na Bukwimba? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli anachosema Mheshimiwa Mbunge na hiyo ndiyo sababu ya mifugo yetu inakosa sifa ya kwenda kuuzwa nje ya nchi kwa sababu haifuati utaratibu unaotakiwa wa Kimataifa. Ndiyo maana Serikali imekuwa ikihamasisha sana mifugo hii iweze kuoshwa katika maeneo mbalimbali na mpango wa Serikali ni kujenga majosho kwa wafugaji wote wanakopatikana ndani ya nchi yetu. Tuko tayari kuja kwenye maeneo hayo aliyoyasema Mheshimiwa Mbunge, kuona kama kuna uwezekano wa kujenga majosho ili mifugo hii iweze kupata hiyo huduma. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Dkt. Chaya.

Na. 687

**Nchi Zinazohitaji *VISA* Rejea Kuingia Nchini**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza: -

Je, ni nchi ngapi ambazo wananchi wake lazima wapate *VISA* rejea kuingia nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54 Rejeo la Mwaka 2016, ikisomwa pamoja na Kanuni za Uhamiaji za *VISA* za mwaka 2016 pamoja na marekebisho yake, Jedwali la Nne la Kanuni hizo limeorodhesha nchi ambazo raia wake wanapaswa kupata idhini ya Kamishna Jenerali wa Uhamiaji (*Visa* Rejea) pindi wanapotaka kuja nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni hizo, kwa sasa ni nchi 27 ndizo wananchi wake wanapaswa kufuata utaratibu wa *VISA* Rejea kabla ya kuja nchini, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, ni nini sasa mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba inakabiliana na wahamiaji haramu ambao kimsingi wamekuwa wakihatarisha sana usalama wa nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa tayari tuna nchi 27 ambazo zinatumia *VISA* Rejea, je, Serikali imeweka mfumo gani wa kuhuisha *VISA* Rejea kwa sababu kuna kipindi tunaona nchi zinaongezeka na nyingine zinapungua? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dkt. Chaya, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati ya Serikali; kwanza iko misako lakini pia iko doria ambayo inafanywa na Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama kuhakikisha kwamba raia au wahamiaji haramu hawaingii nchini. Pia, ipo kauli mbiu kwamba; 'Mjue Jirani Yako,' hii imesaidia sana kuwatambua wahamiaji haramu ambao wanaingia hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, kwanza *VISA* Rejea inatokana na changamoto ya raia wa nchi hizo ambazo nimezitaja nchi 27 lakini pia jukumu hili hufanywa na Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama vya Serikali ya Muungano pamoja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili kuhakikisha kwamba wanatambua viashiria hatarishi kwa wahamiaji haramu hapa nchini, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda.

Na. 688

### Kuchelewa Kujibu Maombi ya Usajili wa Taasisi za Kidini

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA** aliuliza: -

Je, nini sababu ya ucheleweshaji wa maombi ya usajili wa taasisi za kidini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kupewa usajili wa kudumu, taasisi na madhehebu ya dini huwekwa katika kipindi

cha matazamio ili kubaini kama taasisi au dhehebu husika lina dosari yoyote kwa jamii. Hata hivyo, zipo sababu nyingine ambazo huweza kupelekea baadhi ya taasisi na madhehebu ya dini kuchukua muda mrefu kusajiliwa ambazo ni pamoja na kushindwa kutekeleza maelekezo yanayohusu usajili yanayotolewa na Ofisi ya Msajili kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia ofisi ya Msajili wa Jumuiya inaendelea kushughulikia maombi ya usajili wa taasisi na madhehebu ya dini na kutoa usajili kwa wakati kwa taasisi zenye sifa stahiki, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ng'enda.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua kwa nini sasa Serikali haitoi muda maalumu wa kufanya uchunguzi wa taasisi hizo wakati wa maombi na badala yake kuacha inakwenda mpaka miaka mitano wameomba?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, Serikali inafaidika nini na hizi taasisi ambazo zipo zinafanya kazi kwa zaidi ya miaka 20 zinahitaji usajili, kurasimisha tu lakini Serikali inashindwa kufanya hivyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante; ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali la kwanza, tumeweka miaka miwili hadi mitano ili kuhakikisha kwamba kwanza tunazichunguza vizuri taasisi na hii inatokana na unyeti wa taasisi za dini. Lazima tujiridhishe kwamba taasisi zinafanya majukumu ambayo yameorodheshwa kwenye katiba zao na siyo nje ya utaratibu ambao umewekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu jambo la pili, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba taasisi hizi zote za dini zinafanya kazi kwa mujibu wa sheria na kanuni za nchi na hii ni katika kulinda usalama wa nchi yetu. Ziko sababu ambazo zinapelekea baadhi ya taasisi kukaa muda mrefu bila kusajiliwa, kama alivyosema miaka 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa ambazo ziko ndani ya Wizara, kwa sasa kuna taasisi zisizozidi tano ambazo zimekaa muda mrefu. Hii inatokana na kwamba taasisi hizo zinahamahama ofisi. Mara zimesajili kwa kupitia taasisi nyingine wakati zinasubiri usajili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, jukumu kubwa hasa ni kuhakikisha taasisi hizi zinafuata Katiba na sheria za nchi yetu lakini pia kuzingatia usalama wa raia na nchi yetu kwa ujumla. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Maimuna Mtanda; kwa niaba Mheshimiwa Mchungahela.

Na. 689

**Hitaji la Karakana na Mabweni *VETA* – Kitangali**

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA K.n.y. MHE. MAIMUNA S. MTANDA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga karakana na mabweni katika Chuo cha *VETA* Kitangari?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, majengo ya Chuo cha *VETA* Kitangari yalitolewa na Mfuko wa Elimu wa Newala na yalikuwa yanatumika kama majengo ya shule ya Sekondari. Majengo hayo wakati yanachukuliwa na *VETA* yalikuwa chakavu. Serikali ilifanya ukarabati na kujenga upya baadhi ya majengo ili yaweze kukidhi mahitaji ya kuwa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya chuo hiki mwaka hadi mwaka ambapo jengo jipya la utawala lilijengwa na kukarabati baadhi ya majengo ili kupata karakana mbili za ushonaji na umeme na darasa pamoja na bweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya chuo kwa kujenga bweni la wasichana pamoja na nyumba ya Mkuu wa Chuo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/2025 kiasi cha shilingi milioni 100 kimetengwa kwa ajili ya umaliziaji wa miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuongeza miundombinu mingine ya majengo ikiwemo mabweni na karakana katika chuo hicho, ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchungahela. *(Makofi)*

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule hii ina tatizo la walimu, kwa hivi sasa ina walimu sita tu; je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza idadi ya walimu kuondokana na changamoto iliyokuwepo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la walimu limekuwa ni tatizo sugu Mkoani Mtwara kwa ujumla. Je, Serikali ni lini italichukulia tatizo hili kwa umuhimu unaostahili? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mchungahela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tukiri kwamba kuna changamoto ya walimu katika Chuo hiki cha Kitangari na siyo chuo hiki tu bali karibu vyuo vyote kutokana na uongezekaji uliotokea baada ya kujenga vyuo vipya 25 vya wilaya na vile vinne vya mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tarehe 02/03/2024 tumepata kibali cha kuajiri jumla ya walimu 239. Kati ya hao, watumishi 72 ni watumishi mwega na watumishi 167 ni walimu. Tutahakikisha kwamba walimu hawa watakapopatikana tutakipa kipaumbele Chuo hiki cha Kitangari lakini tutawapa kipaumbele sana Mkoa wa Mtwara na vile vyuo vipya 25 vya wilaya na vile vinne vya mikoa, ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, wapeni kipaumbele walimu wanaojitolea. Msitafute walimu wapya wakati walimu wanajitolea miaka minne, saba hawana ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Shigongo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Serikali kwa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Kayenze huko huko Nyehunge. Swali langu ni kwamba, je, chuo hiki ujenzi wake utakamilika lini, maana kwa hivi sasa ujenzi huu unasuasua?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nikijibu swali dogo la Mheshimiwa Shigongo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Serikali inaendelea na ujenzi wa vyuo vya wilaya 64 pamoja na chuo kimoja cha mkoa ambacho ni Mkoa wa Songwe. Moja kati ya vyuo vinavyojengwa ni katika jimbo la Mheshimiwa Shigongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Shigongo na Wananchi wake wa Buchosa; Serikali inaendelea na ujenzi huu kwa awamu na tumekuwa tukipeleka fedha. Tayari tumeshapeleka zaidi ya shilingi milioni 200 na kitu kwa ajili ya ujenzi na hivi sasa tunafanya ununuzi wa vifaa vya viwandani ambavyo ni zile *LGS* au *Light Gauge Steel* pamoja na mabati kwa ajili ya kupeleka kukamilisha ujenzi katika chuo hiki. Ni imani yetu itakapofika mwezi wa kumi au kumi na moja, ujenzi wa chuo hiki utakuwa umekamilika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Festo Sanga.

Na. 690

**Mradi wa Kilimo cha Umwagiliaji – Kitulo**

**MHE. FESTO R. SANGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza Mradi wa Kilimo cha Umwagiliaji Kata ya Kitulo kwa wakulima wa viazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeanzisha mkakati wa muda mrefu wa

kuwawezesha wakulima wadogo wa viazi Mkoa wa Njombe kwa kuwawekea miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba yao. Kabla ya kujenga miundombinu hii, taratibu za kawaida za kujenga mradi huwa zinafuatwa, ikiwemo kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea kutambua maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji nchini, ikiwemo yale yanayolimwa zao la viazi. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, wataalamu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji watatembelea Kata ya Kitulo ili kubaini maeneo yanayofaa kwa shughuli za umwagiliaji na kuyaingiza kwenye mpango wa ujenzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, Kata ya Kitulo ni moja kati ya kata ambayo inaongoza kwa mapato kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Makete kutokana na zao la viazi. Ukulima wao umetusaidia sana kwenye kupata mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ninaomba niulize; ni ipi *commitment* ya Serikali? Mmeonesha kwamba wataalamu wataenda lakini Wananchi wa Kitulo wanatamani kusikia, ni lini mradi wa ujenzi wa skimu ya umwagiliaji utaanza ili na wao waanze kuzalisha mazao *throughout the year*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, nitaanza ziara ya kijiji kwa kijiji katika Jimbo la Makete baada ya Bunge hili la Bajeti. Uko tayari kuongozana na mimi nitakapofanya ziara katika Kata ya Kitulo ili wananchi wapate majibu ya Serikali kuhusu mradi huu ambao ni mzuri kwa ajili ya maendeleo yao? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, cha kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia wananchi wake wa Jimbo la Makete lakini nimwondoe

shaka Mbunge wa Makete. Timu yetu ya wataalamu itafika katika Eneo la Kitulo na wakati wanakwenda tunahitaji tu wananchi wawape ushirikiano na tutakutaarifu Mheshimiwa Mbunge wataalamu watakapofika, nikuhakikishie tu kwamba katika mpango wetu tulionao tutaingiza eneo hili ili walau katika mwaka wa fedha unaokuja ujenzi uweze kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ziara ni hesabu katika moja ya siku utakazozipanga nitakuwa tayari kufika katika eneo hilo na kuzungumza na wananchi wa Kitulo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, swali la Mheshimiwa Malleko litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Mafuwe.

Na. 691

**Mauzo ya Nyama Nje ya Nchi**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE K.n.y. MHE. ESTHER E. MALLEKO** aliuliza: -

Je, upi mkakati wa Serikali kuongeza mauzo ya nyama nje ya nchi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuhakikisha mauzo ya nyama nje ya nchi yanaongezeka. Mikakati hiyo ni pamoja na ukamilishaji wa mkakati wa mauzo nje ya nchi. Serikali kuendelea kuongeza bajeti ya kuboresha sekta ya mifugo, kuvutia uwekezaji wa uongezaji thamani katika sekta ya mifugo, kutumia Balozi zetu kutafuta masoko kwa kufanya majadiliano na nchi zenye uhitaji wa nyama na upatikanaji na ukamilishaji wa michakato ya kupata ithibati mbalimbali zinazokubalika Kimataifa, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali kwa niaba ya Mheshimiwa Esther Malleko. Pamoja na mipango ambayo ameeleza hapa ya Serikali, Serikali inachukua hatua gani za haraka sasa kuhakikisha kwamba tunapata masoko nje ya nchi ikizingatiwa kwamba Tanzania ni nchi ya pili Afrika kwa wingi wa mifugo ili nyama yetu iweze kupata bei iliyo nzuri kwenye masoko ya dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Serikali ilituelekeza Jimbo la Hai kuhakikisha tunaanza kuwekeza pesa kidogo kwa ajili ya kujenga machinjio ya kisasa pale *KIA*. Je, Serikali ipo tayari sasa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Hai kujenga machinjio ya kisasa ili sasa nyama iweze kutengenezwa pale *KIA* na ipakiwe na ndege kwa Mikoa yote ya Kanda ya Kaskazini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kufuatilia kuhusiana na sekta hii ya mifugo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli moja ya hatua tunazozifanya kama Serikali ni kutafuta masoko nje ya nchi na kupitia Taasisi yetu ya Maendeleo ya Biashara Nje *(TANTRADE)*, tumeshaanza kuongea na kuingia makubaliano na baadhi ya nchi nje kwa ajili ya kupata masoko ya nyama ikiwemo Saudi Arabia, Qatar, Iran, China na nchi nyingine. Ambazo hizo kwa mfano, Saudi Arabia tu wanahitaji tani laki saba za nyama ya Ng'ombe kwa mwaka, kwa hiyo tumeshakubaliana nao tutaanza kuendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iran wanataka tani 70,000 kwa kila wiki, sasa tunachokifanya ni kuhakikisha tunawawezesha wananchi wetu wafuge kisasa ili nyama hizi zipate ithibati ili ziweze kuingia kwenye masoko hayo, lakini pia kwenye soko letu la Afrika tayari nako tumeshaanza kuingia ili kupata masoko ya nyama

kwa maana ya kuuza nyama ambayo imechinjwa badala ya kuuza mifugo.

Kuhusu suala la pili ni kweli moja ya maeneo ambayo tunayafanyia kazi ya kimkakati ni kuongeza miundombinu wezeshi ambayo itafanya nyama yetu iwe na ubora unaotakiwa. Moja, ni majosho lakini kama nilivyosema ufugaji wa kisasa na machinjio ya kisasa. Sasa tumeshaanza kukaribisha wawekezaji kwenye machinjio ya kisasa lakini nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa sababu tayari katika Jimbo lake la Hai wameshaanza mchakato wa kujenga machinjio hayo ya kisasa, Serikali italeta fedha ili kuunga mkono machinjio hayo ili yaweze kukidhi ubora wa kutoa nyama yenye ubora kuingia kwenye masoko ya kimataifa, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri hiyo ni mikakati mizuri lakini *walk the talk*, msiseme tu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni wageni waliokaa jukwaa la Spika wageni wa tatu wa Mheshimiwa Spika, Taasisi ya *Miss Travel World 2024*, Ndugu Samwel Mwaligu Rais wa *Miss Travel World Organization* Tanzania. Ndugu Agness Satura, *Miss Travel World 2024* pia mwanafunzi wa Chuo cha Anga cha *Swissport*. Ndugu Anastazia Benard, Mratibu Msaidizi. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, Wageni 53 wa Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Maafisa Tarafa, Watendaji wa Kata na Wenyeviti wa Vijiji kutoka Chamwino Mkoani Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 21 wa Mheshimiwa Omari Juma Kipanga, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Walimu na wanafunzi wa taasisi ya *My Street First* kutoka Kisiwani Mafia, Pwani. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mwenezi wa Kata ya Bumera Jimbo la Tarime Vijijini, Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, ambae ni mpigakura wake na mwanamuziki kutoka Bunda Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Wageni 14 wa Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Mlimba Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Edwin Swalle, wajumbe wa kamati ya maandalizi ya Dar es Salaam *University Students Organization (DARUSO) Legends Retreat*. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Yustina Rahhi, wafanyabiashara kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Mhandisi Isack Kamwelwe, watumishi kutoka Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* Mkoa wa Katavi. *(Makofi)*

Wageni wa nne wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, wajasiriamali kutoka Kigamboni Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni 22 wa Mheshimiwa Phillipo Augustino Mulugo, walimu ambao ni makada wa Chama cha Mapinduzi kutoka Wilaya ya Songwe. *(Makofi)*

Wageni 27 wa Mheshimiwa Francis Mtinga, viongozi wa Chama cha Mapinduzi ambao ni wenyeviti, makatibu wenezi, umoja wa vijana na Katibu wa Mbunge kutoka Mkalama, Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Esther Midimu, Makatibu wa Umoja wa Wanawake kutoka Mkoa wa Simiyu. *(Makofi)*

Wageni nane wa Mheshimiwa Salim Mussa Omar, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)* kutoka Pemba, Jimbo la Gando. *(Makofi)*

Wageni 50 wa Mheshimiwa Jacqueline Kainja, wanakwaya wa Kanisa la *Esaku Anglican* kutoka Urambo Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni Mwalimu Yohana Leguna kutoka Jijini Dar es Salaam, wajasiriamali watano kutoka Jijini Dodoma, wanafunzi 100 na walimu 10 wa shule ya Msingi Yakini kutoka Jijini Arusha, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 40 wa jukwaa la kushughulikia mahitaji ya wasichana wa Kiislamu, wanawake na vijana nchini Tanzania *(Ladies in Islam)* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Shangazi, Katibu wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, anaomba kuwatangazia wabunge wote CCM, kuwa kutakuwa na *Party Caucus* leo Saa Saba, mara baada ya kusitishwa shughuli za Bunge, katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaanza na Mheshimiwa Kunambi, ajiandae Mheshimiwa Makoa, ajiandae Mheshimiwa Munde Tambwe.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nimi nijielekeze moja kwa moja kwenye hoja iliyopo

mezani. Nimetumia muda mrefu kusoma Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Nilijipa muda pia wa kupitia bajeti yetu na sasa naomba nichangie.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo naomba niliweke bayana hapa kupitia kwenye mpango huu, bahati nzuri Profesa Kitila ni Kaka yangu na ni rafiki yangu wa karibu, sasa katika mambo ambayo ninaweza kuyasema leo hii, nilichokiona kipya, maana yake awali niliwasifia lakini leo napata mashaka kidogo. Katika mpango huu nilichokiona kipya pekee ni kwamba kuanzisha kitu kinachoitwa *KPI (Key Performance Indicators)* hii ndiyo jambo jipya, kinyume cha hapo kwenye huu mpango ni kazi iliyofanywa ya kukusanya taarifa za Wizara zote na kuweka kwenye kitabu kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikapata mashaka kidogo leo kumetokea nini, kaka yangu Mkumbo na ameingia kwenye mtego wa namna hiyo, sasa naomba niseme machache kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo awali namshukuru sana Mheshimiwa Jenista Mhagama, akiwa Waziri wa Utumishi na Utawala Bora, niliwahi shauri Serikali namna gani tunaweza kuachana na mfumo wa *OPRAS* na tukaja na mifumo ambayo itaweza kupima watumishi wetu wa umma na taasisi zake za umma. Serikali ilisikia mchango wangu na ikabadilisha ikaachana na *OPRAS* ikaja na mfumo wa *PEPMIS* na *PIPMIS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *PEPMIS* kwa maana ya *Public Employees Performance Information System* (Mfumo wa Upimaji Utendaji Kazi wa Utumishi wa Umma) na *PIPMIS* kwa maana ya *Public Institutions Performance Information System* (Mfumo wa Upimaji wa Utendaji Kazi wa Taasisi za Umma). Kilichosahaulika ni *PEPMIS*, namshukuru Mungu leo kuona kwenye mpango, Mheshimiwa Waziri wa Mipango kaleta *KPI*. Sasa jambo hili nimshauri pia Waziri mwenye dhamana ya Utumishi na Utawala Bora wa sasa, Mheshimiwa Jenista aliweza kukubaliana na hoja ya kuachana na *OPRAS* akaja kwenye mifumo hii ya upimaji utendaji kazi wa watumishi wa umma na taasisi. Sasa Mheshimiwa

Simbachawene Kaka yangu ni muhimu sasa ukawa pamoja na Waziri wa Mipango kwenye mfumo huu wa *KPI*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *KPI* ndiyo inayoweza kupima utendaji kazi tunafahamu, ngazi ya Wizara Mawaziri wanapimwa na vyombo lakini *KPI* ni mfumo mzuri na watanzania wangejua. Kwa hiyo *KPI* ikianza kwenye ngazi za Wizara, Mkoa mpaka Wilaya, Wakuu wa Wilaya pia wapewe *KPI*, Wakurugenzi wa Halmashauri wapewe *KPI*, hii itatusaidia kuamsha ari ya utendaji kazi wa watumishi wetu wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa nini nimesema eneo hili ninampongeza, kwa sababu mimi nafahamu eneo hili linakwenda kubadilisha fikra na tabia za mazoea kwa Wakuu wa taasisi za umma kufanya kazi kwa mazoea.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa pili ninasema tu, Kaka yangu Kitila umeingia kwenye mtego ambao sikutegemea uingie, umeweka *KPI*, nilikuwa naangalia sekta hii ambayo nina maslahi nayo mapana sekta ya ardhi. Nimesoma kwenye mpango wako kwenye sekta ya ardhi umeeleza pale nikawa najiuliza hii kama ni *copy* na ku-*paste*, kwa sababu sijaona unakwenda kumpimaje huyu Waziri wa Ardhi, mwisho wa siku kwenye utekelezaji wa majukumu yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalani naomba ninukuu ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2020/2025, ilani inaelekeza kwenye Sekta ya Ardhi, kwamba inaelekeza Serikali kupanga matumizi bora ya ardhi katika Wilaya 54 zenye miradi ya kimkakati pamoja na vijiji 4,131. Baadaye inaendelea kusema kwamba, kusimamia na kuratibu uandaaji wa ukamilishaji wa mipango kabambe *(Master Plan)* ya Miji mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa mpango huu unampimaje huyu, unampimaje? Kwa sababu naona kilichowekwa humu ni taarifa yake yeye kuja kwenye mpango! Sasa ninakuomba huu mtego Kaka yangu nakuamini sana uwezo wako, niombe hapa usiingie kwenye huu mtego wa kukusanya

taarifa za Wizara mbalimbali na ku-*compile* kwenye kitabu kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mipango jukumu lake ni kuainisha malengo na kukabidhi Wizara za Kisekta, halafu unapima kupitia malengo uliyotoa kwenye Wizara za Kisekta, hiyo ndiyo unaweza kumpiama. Sasa nimeeleza hapa kwa habari ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi, sasa je, vijiji elfu nne na kitu vyote vipimwe unampimaje na sasa tumebaki mwaka mmoja? Kwa hiyo, ninakushauri tu kwamba unakwenda eneo ambalo nadhani linaweza likashindwa kutusaidia Watanzania kwenye Wizara yako ya Mipango na Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine niendelee kwenye eneo la bajeti yetu. Nchi yetu wote tunafahamu ni nchi maskini, sasa kupanga ni kuchagua, napata changamoto kweli, kama nchi hii inachangamoto ya miundombinu ya barabara kila kona, kila kona barabara ni shida, hivi ni kweli tunakwenda kupeleka shilingi trilioni sita kujenga viwanja vya ndege? Barabara ndiyo siasa, sasa niwaombe Wabunge wenzangu na niiombe Wizara ya Fedha katika hili. Nitoe mfano, leo hii unajenga kiwanja cha ndege Shinyanga, Mwanza *to* Shinyanga kilometa 150. *Viability of the project, investment Vis-à-Vis viability* tunataka ku-*achieve* nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo fedha inayopelekwa pale ingejenga barabara ngapi nchini, sasa nimezungumza hapa kupanga ni kuchagua. Kwa hiyo ndugu zangu Wabunge wote humu tunazungumza barabara, wanaozungumza viwanja vya ndege nadhani ni wachache sana, hivi hatuwezi kutafakari katiki hili? Kwa hiyo, nachelea kuunga mkono hoja hasa Wizara ya Fedha, kama mimi barabara yangu ya Morogoro - Njombe *border*, mikataba imesainiwa kilometa 100 mpaka leo Mkandarasi hajapewa fedha malipo ya awali tu shilingi bilioni tisa hajalipwa, leo nikubali kujenga viwanja vya ndege kwa wengine, nikubaliane na hoja ya Wizara ya Fedha, sitawatendea haki wananchi wangu wa Mlimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo katika hili siungi mkono hoja ya Wizara ya Fedha mpaka nione kwenye majumuisho Waziri wa Fedha ameainisha namna gani anakwenda kuachana na vitu, lazima tuchague barabara ndiyo msingi wa wananchi wote nchini. Kwa hiyo kwa habari ya viwanja vya ndege sisemi visijengwe, tusubiri kidogo tukamilishe barabara, kwa sababu nchi nzima kuna kero za barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine niende kwenye sekta ya mifugo, samahani naomba niseme...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kengele ya pili, tunachangia kwa dakika nane leo. *(Kicheko)*

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga hoja Mpango lakini bajeti ya Wizara ya Fedha nadhani mpaka *clarification* ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Makoa, jiandae Mheshimiwa Munde. Mheshimiwa Makoa hayupo Mheshimiwa Munde.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipo. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu na nishukuru kwa Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutekeleza miradi katika nchi hii. Ninaanza na kuunga mkono hoja iliyopo mezani, nina michango michache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Serikali imefanya mambo makubwa katika bajeti hii ambayo tunaendelea nayo na mwaka wake unaisha wiki moja ijayo, kwa maana hiyo tunaimani kubwa sana na bajeti hii ambayo tunakwenda kuipitisha na kutokana na hilo sasa ndiyo maana nikaunga hoja, nikaunga mkono hoja mapema kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepeleka fedha nyingi sana kwenye Majimbo yetu katika kutekeleza miradi na hivyo tunayo imani kubwa hata mwaka ujao wa fedha kasi na mwendo utakuwa ni huo huo na hivyo kuendelea tu kuisisitiza Serikali

kuhakikisha fedha ambazo tunazipitisha kwenye Bunge hili ziwafikie wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona juhudi za Serikali hata katika bajeti hii kwa mfano, tulipangiwa visima vitano katika kila Jimbo na tumeona Wizara imeshapeleka wataalamu na tayari maandalizi ya kuanza kutekeleza miradi hii yameanza. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali lakini pia hata katika shule ambazo tumepangiwa na Serikali katika bajeti hii ambayo tunakwenda kuipitisha nimeona maandalizi kwamba wameshaanza kwenda kuangalia maeneo na kujiridhisha ili waweze bajeti ikipita hii waweze kupeleka fedha haraka na kwenda kutekeleza miradi, hiyo napongeza sana Serikali na nina imani kubwa na Serikali yangu iliyo chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba katika kipindi hiki cha mwaka tumefanya miradi mingi na miradi mingi bado haijakamilika. Kwa mfano, miradi ya maji, sehemu kubwa ya miradi ya maji bado ipo kwenye utekelezaji na mwaka wa bajeti ndiyo huu unakwisha, ninaiomba Serikali kuhakikisha ile miradi yote tuliyoanza nayo yenye miaka mitatu, miaka miwili ama mwaka basi katika kipindi hiki tunachoelekea bajeti inayofuata basi miradi ile iende ikakamilishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukimalilisha ile miradi ndipo tutakapoanza na miradi mingine. Kikubwa ninachosisitiza hapa ni kwamba matokeo ya fedha ya Serikali yatakamilika tu pale ambapo wananchi wataanza kupata huduma kupitia ile miradi. Kwa maana hiyo nina imani na ninaamini kwamba kwa sababu imekuwa ni kilio cha Waheshimiwa Wabunge juu ya miradi yetu hii ambayo imekamilika, basi Serikali itaweka mkazo kulipa madeni ya wakandarasi pamoja na kumalizia viporo vilivyobaki nyuma kabla hatujaanzisha miradi mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nazishauri Wizara zote kwa ujumla zishirikishe Wabunge ili pasiwe na changamoto katika kutekeleza miradi hiyo. Nimeona mfano hapa wa haya maeneo ya sekondari; wataalamu walipokwenda kwenye jimbo langu kuyaangalia wakakutana na changamoto. Wamekwenda bila

kutoa taarifa kwa mwenye jimbo, lazima utapata changamoto. Wamekwenda kuoneshwa maeneo wakayakataa maeneo, maeneo ambayo unakuta ni maeneo ya milima; na kweli ukiweka fedha ya Serikali kujenga shule maana yake shule haitakamilika, bajeti ndiyo hiyo ilipangwa, tutaanza kuisumbua tena Serikali kwenda kutafuta fedha ambazo hazikuwepo kwenye mpango ili kukamilisha zile sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo nimeona barua za kuyakataa yale maeneo, lakini nilipigiwa simu na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, nikamwambia Jimbo la Kondoa Mjini wazee wanamwamini sana kijana wao. Kama tatizo ni eneo katika sekondari zote tulizozijenga wazee walinikabidhi mimi maeneo, kwa sababu wana imani. Hata walipokwenda wakakwama maana yake ni kwamba, wamekwama kwa sababu hawakumshirikisha mwenye jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtoe hofu Mheshimiwa Waziri, tayari wazee wamenipigia simu kwenda kunionesha maeneo mazuri kwa ajili ya ujenzi wa miradi hiyo ya sekondari mbili; Sekondari ya Kingale na hiyo tunayokwenda kuijenga kule Suruke. Kwa maana hiyo mpango huo wa fedha wasije wakakwama kupeleka kwa sababu ya kuwa na mashaka na maeneo. Ninawatoa mashaka, mpango uendelee vizuri, nina hakika ndani ya wiki hii nitakamilisha utaratibu mzima wa hayo maeneo na nitailetea Serikali ili iweze kutekeleza miradi kwa ajili ya wananchi wa Kondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalolisisitiza ni kwamba, tuna jambo kubwa sana la ujenzi wa lile Daraja la Mto Bubu, kila siku tunaliongelea jambo hili. Lile daraja likijengwa litakuwa ndio uchumi wa watu wa Kondoa. Kwa hiyo, kwa sababu tayari taratibu za awali zimekamilika ninaiomba Serikali ianze kuona namna ya kupeleka fedha kwa ajili ya kuanza kujenga Daraja lile la Munguri B; tumezoea kwa kusema ni Daraja la Munguri. Baada ya kuyasema hayo ninaunga mkono hoja. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munde, wajiandae Mheshimiwa Kilumbe na Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato. Mheshimiwa Munde, hayupo. Mheshimiwa Kilumbe, wajiandae Mheshimiwa Dkt. Nahato na Mheshimiwa Profesa Shukrani.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii. Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya na uzima. Nitumie nafasi hii vilevile kuendelea kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya uongozi wa kipenzi chetu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ya maendeleo inayoendelea kufanyika kwenye majimbo yetu kote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu leo nataka nijielekeze kwanza kabisa katika ugawaji wa fedha kwenye miradi ya maendeleo. Moja ya tatizo ambalo tunakutana nalo sisi kama Waheshimiwa Wabunge ni suala zima la usawa na haki katika ugawaji wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba siku zote bajeti haitoshi, tuna mahitaji makubwa lakini kipato chetu ni kidogo; lakini tunataka hicho kidogo kigawanywe kwa usawa. Leo hii ni miaka mitatu sasa Serikali inatenga bajeti ya kukarabati Meli ya Liemba na Mwongozo bila kupeleka fedha na bila mradi kutekelezwa; sasa hii haiwezi kuwa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo ipo miradi ya mabilioni kwa mabilioni inafanyika, lakini hii miradi midogo tu kwa ajili ya maendeleo ya wananchi kwenye maeneo hayo haifanyiki. Kwa hiyo, nitapenda Waziri wa Fedha atakapopata nafasi atueleze Wizara yake inaweka *priority* gani katika ugawaji wa fedha na kusahau kabisa mambo ya msingi kama haya kwenye baadhi ya maeneo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ninalotaka kuzungumzia ni kuongeza wigo wa kodi na tozo. Kwa mfano, hapa tulikaa kuzungumza katika Bunge hili tukatazama kitu kinaitwa *capital gain tax…*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaomba utulivu ndani ya Bunge.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tulikaa katika Bunge hili tukazungumzia kitu kinaitwa *capital gain tax* ambacho kilikuwa kinatozwa asilimia 10. Mtu anauza nyumba yake kwa shida lakini anatakiwa apeleke asilimia 10 ya mauzo yake kwa Serikali. Serikali ikasikia hoja za Waheshimiwa Wabunge ikashusha kutoka kwenye asilimia 10 mpaka asilimia tatu. Ninaipongeza sana Serikali, na ninafikiri na wenyewe wanaona namna ambavyo watu sasa hawakwepi *capital gain tax. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado kuna tatizo kwenye *withholding tax* ya *rental*. Watu wenye nyumba za kupangisha sasa wamekuwa wengi na *apartments* zimekuwa nyingi, lakini wengi bado wanakwepa kulipa *withholding tax* kwa sababu bado mmeacha asilimia 10 kwenye *withholding tax* ya *rental*. Mimi nilipwe kodi ya nyumba 2,000,000 nichukue 200,000 nipeleke Serikalini. Tulitazame tena eneo hili. Unapotaka kuongeza wigo wa walipa kodi unachokifanya ni kuangalia wingi wao kisha unapunguza ile kodi ili walipe wengi badala ya wengi kukwepa kodi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili nilitaka nije hata kwa bodaboda. Leo uchunguzi unaonesha kwamba asilimia takriban 80 ya bodaboda hawana leseni; na hawana leseni si kwa sababu wanapenda, hawana leseni kwa sababu kipato chao ni kidogo na leseni ni bei kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachanganya haya mambo, hawa wanaoendesha vyombo vya moto wamegawanywa katika mafungu duniani kote. Anayerusha ndege juu anaitwa *pilot* ambaye sisi tunamwita rubani, ana leseni yake. Anayeendesha meli anaitwa *captain* sisi tunamwita nahodha, ana leseni yake. Anayeendesha treni ana leseni yake anaitwa *operator* maana treni ni kama vyombo vingine, ni kama *grader* ni kama nini wanaitwa ma-*operator*. Anayeendesha gari anaitwa dereva,

anayeendesha pikipiki haitwi dereva anaitwa *rider.* Leo hatuna leseni ya *rider* tunampa *driving license,* ambayo ni ya mwendesha gari, kwa ku-*categorize* tu. Kwa hiyo mimi ninachoomba sasa ni kwamba Serikali ije na leseni za *rider,* kuwe na *riding license* ambayo kiwango chake kiwe shilingi 20,000. Hawa asilimia 80 wote ambao walikuwa hawalipi sasa watalipa na tutapata fedha nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unakumbuka Bunge hili kwa kuangalia uzito na kipato cha kila eneo tuliiomba Serikali na Serikali hii ni sikivu ikaamua hata makosa ya barabarani, haya ya magari yanatozwa 30,000 kwa kila kosa lakini ya pikipiki Serikali ikasikia ikaleta hadi shilingi 10,000. Vilevile leseni kwa ajili ya *rider* iwekwe shilingi 20,000, watalipa wengi tutapata fedha nyingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nimalizie suala la kuipongeza Serikali kwa kuangalia jinsi ya kuongeza mapato ya kikodi kwenye nishati ya gesi. Hili ni eneo ambalo mmeliangalia na mimi kwa kweli naunga mkono. Isipokuwa, siungi mkono kabisa kabisa hoja ya kutoza kodi kwa *AMCOS.* Hawa ni wakulima tena wakulima ambao sisi tunajua namna ambavyo wanapata shida kubwa sana na vilevile mazao yao hayana uhakika wa bei. Kila mwaka wanaomba Mungu sijui watakutana na kitu gani huko mbele; sasa wamejiunga katika ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tufike mahala tuangalie maeneo haya niliyoyataja ambayo yanaweza yakatuongezea kodi kwa kiasi kikubwa. Kwenye *withholding tax* ya *rental* kwenye gesi, sawa lakini kwenye *AMCOS* hapana. Yaani hawa watoto wanaanza kuinuka tu; umezaa mtoto umemuona tu anaanza kupendeza unaanza kumtafutia mchumba, haiwezekani. Suala la msingi hapa tuache ushirika ukue kwanza. Baada ya kusema hayo. Ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe, ahsante. Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato, jiandae Mheshimiwa Profesa Shukrani.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika Bajeti hii Kuu ya Serikali. Awali ya yote napenda kumshukuru sana Mungu kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kusimama leo na kuchangia katika Bajeti hii Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza sana Serikali kwa jinsi ambavyo imeweza kuwasaidia vijana wetu, hasa wa vyuo vikuu kwa kuwapatia mikopo na fedha nyingi sana na kuwawezesha vijana wengi sana wa Kitanzania kupata fursa ya kusoma katika vyuo vyetu vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo hii ya vyuo vikuu imekuwa msaada mkubwa sana tangu imeanza kupatikana katika nchi hii ya Tanzania. Wengi tuliosoma katika vyuo vikuu hivi tupo hapa kwa sababu ya hii mikopo. Hivyo, basi, mimi niendelee tu kuisisitiza Serikali yetu sikivu iwapatie wanafunzi wetu mikopo kwa wakati sahihi, na wale waliojipambanua kwamba wanahitaji hii mikopo kamili wapate kwa asilimia 100 na kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee pia kuipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo inaendelea kuboresha miundombinu katika vyuo vyetu vikuu majengo yajengwa, vyuo vikuu vingi vinapata miundombinu mizuri sana. Sasa naomba leo mchango wangu nijikite katika kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundisha katika vyuo vyetu vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, udahili wa vyuo vikuu umeongezeka, na hii imetokana na uboreshwaji wa elimu katika nchi yetu. Sekondari zimejengwa nyingi na wanafunzi wengi sasa wamehamasika kusoma. Kwa hiyo, wanafunzi hawa wanakuwa na ndoto nyingi sana za kufika vyuo vikuu. Hivyo basi, ni vizuri sasa Serikali ikaangalia jinsi ya kuboresha vyuo vyetu vikuu ili viwe tayari kuwapokea hawa wanafunzi wengi ambao wanakuja katika miaka ya hivi karibuni. Kwa sasa hivi kumekuwa na ongezeko kubwa sana la wanafunzi, takribani 150,000 wanajiunga na vyuo vikuu. Udahili huu ni vizuri ukaenda sambamba na miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua ya kwamba ardhi inabaki pale pale lakini wananchi wanaongezeka. Hali kadhalika ndivyo ilivyo katika vyuo vikuu. Vyuo vikuu vipo pale pale lakini wanafunzi wanaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali halisi iliyopo sasa hivi ni kwamba miundombinu ya vyuo vikuu vingi hasa vya umma haiendani sambamba na uongezeko la wanafunzi. Hapa tunamaanisha miundombinu kama mabweni. Ni hivi, vyuo vyetu vikuu sasa vinapokea asilimia 30 tu ya wanafunzi wanaolala katika mabweni ya vyuo vikuu, wanafunzi wengine wanalala nje, hii ni changamoto. Wanatafuta vyumba nje ya vyuo vikuu ambavyo vinakuwa mbali huku wanafunzi wakikumbana na changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikichukulia mfano wa Chuo Kikuu cha *MUHAS* wanafunzi wengi wanakaa mbali na hivyo wanakumbana na changamoto za usafiri na vilevile wanakumbana na changamoto za kuishi nje ya chuo. Hivyo, wanakuwa na changamoto ya kuwa vizuri katika masomo yao na hutumia muda mwingi katika kufikiria mambo mengine nje ya masomo yao. Hivyo basi ninaishauri Serikali katika bajeti hii ijaribu kuongeza vyumba vya mabweni katika vyuo vyetu vikuu ili wanafunzi waishi katika sehemu ambazo zinaeleweka, wapate mahitaji yao katika sehemu inayoeleweka na waweze kujifunza masomo yao na kuyazingatia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuhusiana na kumbi za mihadhara katika vyuo vyetu vikuu; ni kwamba wanafunzi wanaongezeka lakini kumbi za mihadhara ni zile zile na zikiongezeka hali kadhalika haziendi sambamba na uwiano wa wanafunzi. Kumbi za mihadhara ndizo sehemu ambako pia wanafunzi wanafanya mitihani yao ile ya *monthly test, quarter test*. Sasa wanafunzi ni wengi sana katika kumbi hizi, hata mhadhiri kuwasimamia inakuwa ni ngumu kuhakikisha kwamba kweli mwanafunzi anafanya hii mitihani peke yake bila kupata usumbufu mwingine wa kuwa karibu na mwingine wakati wa mitihani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika labda niseme tu kwamba kuna suala la motisha kwa wahadhiri wetu, jambo hili ni changamoto. Ninaishukuru sana Serikali angalau safari hii ongezeko na madai ya wahadhiri wetu imetimizwa, na wahadhiri kwa kweli wanaishukuru sana Serikali kwa kupata malimbikizo ya mishahara yao, na hata wale wanaostaafu kupata stahiki zao kwa wakati. Ninaishauri Serikali jambo hili liwe endelevu, lisiwe tu suala la kipindi fulani halafu kipindi fulani wahadhiri hawapati malimbikizo yao ya mishahara au stahiki zao zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kuhusu ofisi za wahadhiri; Serikali iliangalie jambo hili. Maprofesa siyo sahihi kabisa kukaa chumba kimoja na wahadhiri wengine. Maprofesa ni watu ambao wana kazi nyingi, hawa maprofesa wanafanya utafiti, hawa maprofesa wanafanya machapisho mbalimbali na hawa maprofesa ndio ambao wanafunzi wa *Masters* na *PhD* huwaona mara kwa mara kwa ajili ya kuweza kupata *consultation* ya kuwaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wanapokuwa katika ofisi ambazo zimechanganyikana na wahadhiri wengine ni changamoto. Huyu mhadhiri anataka *document* zake zikae vizuri katika ofisi yake, ahakikishe kwamba vitabu vyake vipo. Si vyema maprofesa jioni kuanza kukusanyakusanya vitu vyao na kwenda navyo sehemu nyingine. Kwa hiyo, naomba nishauri sana Serikali iangalie kwa kuhakikisha wahadhiri wanakaa katika ofisi nzuri na ambazo zinaweza kukidhi mahitaji yao kulingana na taaluma zao. Ahsante sana; nami ninaendelea kuishukuru Serikali na ninaunga bajeti hii mkono kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha, wajiandae Mheshimiwa Tauhida na Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi nichangie hoja ya Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango katika Bajeti Kuu ya Serikali. Nitangulie kusema kwamba ninaunga hoja mkono bajeti hii ipite, ila naomba nisiunge hoja mkono katika hoja ya kuweka

kodi katika gesi asilia inayotumika katika magari. Ninaunga hoja mkono bajeti lakini katika hili siungi hoja mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii ya matumizi ya gesi asilia katika magari bado ni changa na haiwezekani sekta changa uanze kuiwekea kodi. Maana yake ni kwamba itakuwa ni kama kujipiga risasi mguuni, na kwa jinsi hiyo kujipungunzia mwendo katika safari ya matumizi ya nishati safi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha utakapokuja kuhitimisha tafadhali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mapendekezo yangu binafsi kodi hiyo kwenye matumizi ya gesi asilia katika magari iondolewe. Kwa sababu magari ambayo sasa hivi yanatumika ni magari madogo madogo ya *uber,* hata haya *light vehicles* hayajaanza kutumia. Kwa hiyo, tunataka kuwa-*tax* wanaotumia *uber?* Hapana. Hiyo kodi ninasema iondolewe na wala siungi hoja mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze katika…

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunapambana kupata *clean energy,* na unapoongezea kodi kwenye gesi tayari una-*encourage deforestation* mahala ambapo tulikuwa tumekwishaanza kuhama. Naunga mkono hoja hii, ninamjulisha mwongeaji kwamba na mimi tutasimama pamoja na yeye ili kuzuia kabisa jambo hili lisitokee. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa, taarifa hiyo?

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipokea. Ninaendelea kusisitiza kwamba hoja ya kuweka kodi katika gesi asilia ya magari *no. It is a big no.* Hiyo iondolewe.

Nakushukuru sana, Mheshimiwa Askofu Gwajima, kwa *support*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze katika Mpango, na Mpango wetu wa Tatu wa Maendeleo ambao sasa unatekelezwa, una vipaumbele ambavyo mojawapo ni kuendeleza rasilimali watu na Mheshimiwa Waziri amekiri kabisa kusema kwamba rasilimali watu ni nguzo katika kujenga uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunatambua kwamba rasilimali watu ni nguzo, ninaomba tunapokwenda kutekeleza bajeti hii twende tukaufanye utumishi wa umma uwe wa kuheshimika. Twende tukaufanye utumishi wa umma uweze kuwa na watu waliokuwa na hamasa ya kazi na motisha ya kufanya kazi. Katika hili tujenge utaratibu wa mwendelezo wa utekelezaji wa maono, njozi pamoja na mipango mikakati ya Wizara pamoja na taasisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuta kwamba kiongozi fulani hivi anakaa katika nafasi yake ya maamuzi kwa muda wa mwaka, anaondolewa, miaka miwili anaondolewa. Sasa tunasukumaje maendeleo iwapo hakuna muendelezo na mara nyingi kunakuwa na kukatikakatika kwa kuendeleza mipango ya taasisi husika. Lakini pia wakati mwingine, mtumishi anapoonekana kwamba ana ujuzi na uwezo mzuri mara nyingi hapewi nafasi, ataondolewa na utamkuta mtumishi huyo anapelekwa mahali ambapo hata si eneo lake la umahiri, na hii imekuwa ikikatisha tamaa sana watumishi na kwa jinsi hiyo wanashindwa kuwa sehemu ya kusukuma mbele gurudumu la maendeleo na kukuza uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jinsi hiyo naomba tunapoendelea kutekeleza bajeti hii hebu watumishi wa umma wapewe nafasi yao ya kufanya maendeleo yao ya nchi kwa kukaa katika nafasi hizo lakini pia kupewa heshima ya utumishi na wala sio kubezwa wakati mwingine kwa sababu wameonekana kwamba wana ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine napenda kuchangia kuhusu mpango wetu unatamka habari ya kwamba kuangazia maendeleo ya viwanda kama sehemu ya kukuza uchumi. Pamoja na kwamba Serikali sio ambayo inayojenga viwanda, lakini ningetamani kuona kwamba mwaka wa fedha unapoanza, Serikali ifanye *survey*, tathmini ya kuona kwamba ni viwanda vingapi, katika maeneo gani tunavitarajia. Hii sentensi ya ujumla ujumla tu kwamba maendeleo ya viwanda na hatujafanya *survey* ni kwamba hatujajipa kipimo fulani ambacho mwaka unaokuja tutajipima kwamba tulipanga kuwa na viwanda kadhaa katika maeneo kadhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hatuweki mkazo huo maana yake ni kwamba mwisho wa mwaka hatutaweza kujipima. Kwa hiyo, ningetamani sana Mheshimiwa Waziri wa Mipango inapokuja katika maendeleo ya viwanda awe ameshafanya *survey* maoteo ni yapi ili tunapofika mwisho wa mwaka tuseme tulitamani viwanda 50 katika maeneo kadhaa; je, tulifikisha lengo au hatukufikisha? Lakini tukienda kwa ujumla jumla hivi itafika mwisho wa mwaka hatuwezi kujifanyia tathmini ya kile ambacho tumekipanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika mojawapo ya viwanda ambavyo mpango umevizungumzia na nanukuu maelezo ya Waziri Prof. Mkumbo kwamba, "tusipoteze nafasi ya kuwa na kiwanda cha kutengeneza betri za magari ya umeme kwa sababu malighafi ya madini ya *Nickel graphate* na *rare earth* itachimbwa hapa siku za karibuni". *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba sana katika hili Serikali ifanye kila inaloweza kuvutia teknolojia hii mahali hapa. Yawezekana tukasema lakini tukashindwa kutekeleza, kwa sababu gani? Wachimba madini mara nyingi wana *offtake agreements,* anachimba kwa sababu anajua mnunuzi yupo wapi? Kwa hiyo, isije ikafika wakati anasema mimi ninachimba kwa sababu wanunuzi wangu wapo na hivyo anapeleka nje. Kwa hiyo, Serikali ifanye kila inaloweza, kuhakikisha kwamba inavutia kiwanda hiki hapa ili sisi Tanzania na nchi nyingine za Afrika

zisiendelee kuwa mahali ambapo madini yanakuwa malighafi kwa ajili ya viwanda vya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaposema kwamba Serikali ifanye kila inaloweza maana yake ni kwamba Waziri wa Mipango, Waziri wa Madini na Mheshimiwa Rais na watu wengine wote ambao ni wahusika wafanye kila wanaloweza ili kuweza kuvutia kiwanda hiki na hatimaye isije ikawa ni *missed opportunity*. Isije ikawa ni nafasi ambayo tena tutaona malighafi zetu za madini zinatumika kwa ajili ya kupeleka nje ya nchi na kuwanufaisha watu wengine. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Profesa.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, haa! Muda umeisha? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tauhida Gallos ajiandae Mheshimiwa Angelina Mabula, ajiandae Mheshimiwa Nusrat, ajiandae na Mheshimiwa Mafuwe. Mheshimiwa Tauhida

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali. Kwanza kabisa nianze kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya ndani ya Tanzania. Sisi kama wanadamu neno kubwa la kumwambia ni ahsante na tunamshukuru kwa mambo mema anayotutendea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukuwe fursa hii kuipongeza Wizara ya Fedha, kumpongeza Waziri wa Fedha na Naibu wake lakini pia na Waziri wa Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuipongeze bajeti yetu ni nzuri na bajeti imewalenga hasa watu wa chini. Katika bajeti yetu kitu ambacho nitaenda kukiongelea kikubwa ni suala la elimu kwa Watanzania, bajeti yetu ni nzuri, fedha zinakusanywa na tunaona

namna miradi inavyotekelezwa, na makusanyo yanakwenda vizuri. Lakini tuiombe Serikali yetu, tatizo kubwa la Watanzania kutokuwa na elimu, wengi wao ninadhani kwamba hawatambui fedha ambazo Serikali inazozitumia kwenye miradi mbalimbali inapata wapi fedha hizo? Ninadhani kwamba, kama Serikali itawekeza zaidi kwenye suala zima la kutoa elimu kwa Watanzania kuonesha namna gani Serikali inaweza kupata fedha na kutekeleza miradi ya wananchi, imani yangu kubwa kwamba, wananchi na kwenye suala la utekelezaji wa makusanyo tutazidi kupanda zaidi ya hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Watanzania kwenye suala la ukusanyaji wa mapato bado elimu kwao ni ndogo. Rai yangu kwa Serikali, maoni yangu kwa Serikali, natamani sana kuona kwamba mkakati wa muda mfupi uliopo bado hatutoweza, kila siku tutakuwa na kazi ya kuelimisha Watanzania kwenye suala la ukusanyaji wa mapato lakini kama tukianza kujipanga na kujisahihisha, wapi kama Watanzania tunakosea, wapi kama sisi viongozi tunakosea, eneo kubwa ambalo tumeshindwa kuwekeza ni kwenye kuwekeza kwenye elimu kwa Watanzania, ili uweze kupata kile ambacho tunakitaka lazima tuwekeze kwenye elimu. Wananchi wa Tanzania uelewa wao kwenye suala la kodi umekuwa wa tofauti. Kama sisi Watanzania na viongozi tukiamua kusema tuanze kuwekeza chini, naamini kwamba kwa miaka ijayo, miaka kumi na tano, ishirini Tanzania itakuwa haina shida kwenye suala la makusanyo ya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwenye upande wa dini ya kikristo wanaanza kumwekeza mtoto kwenye *Sunday school* kuanza kumfundisha mapema kuelewa dini yake, lakini kwenye upande wa dini ya kiislamu mtoto anaanza kupelekwa chuo madrasa ili mtoto aanze kupandikiza zile mbegu mapema na mtoto anapokuwa anakuwa anajielewa kwamba yeye ni nani na yupo wapi, na hili suala la Tanzania kwenye ukusanyaji wa kodi lazima tukubali, ndani ya shule toka mtoto yupo mdogo aelimishwe nini maana ya kulipa kodi, na namna ya kumfundisha mtoto ni njia ndogo tu kwamba ukinunua, ukichukuwa ukipewa risiti inamaanisha kodi inakusanywa ndani ya Serikali, wewe

utapata madaftari, wewe utapata sare za shule utaendelea kusoma bure wewe na wanaokuja pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninadhani sasa ni muda wa Serikali kuwekeza kwenye elimu, tuwekeze kwenye elimu na uelewa uliokuwepo ndani ya Taifa letu ni mdogo. Hata leo ukisikia migogoro iliyokuweko ya wafanyabiashara tatizo elimu tu, uelewa umekuwa mdogo kwenye suala la ulipaji wa kodi. Tuangalie nchi za wenzetu, leo akija mgeni ndani ya nchi ya Tanzania, siku moja nilikutana na mzungu anakuja amemaliza kununua kitu amepewa risiti anaichunguza risiti. Anaulizwa unaichunguza nini anasema nataka nione kodi ya Serikali ipo wapi kwenye risiti? Tunatamani na sisi kama Tanzania wananchi wanaoishi ndani ya Tanzania tuwe na uelewa mmoja kwenye suala la ulipaji wa kodi. Kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Waziri, tutatumia muda mkubwa ili Taifa litukumbuke, lazima tukumbuke kuanza na vizazi vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tukiwa kama viongozi tuanze na watoto wetu majumbani kuwaelimisha nini faida ya kulipa kodi. Pia tuwe na mikakati maalumu kuweka vitu kama hivi vidogo ndani ya shule zetu tukasema labda leo kuna kipindi mwisho tunaelimisha kuhusu suala la ulipaji wa kodi. Ni kitu kizuri, tutakuwa na kizazi ambacho kinaelewa nini maana ya kulipa kodi na kila anayekuwa anaelewa kwamba ili Taifa litumie, ili Serikali iwe na mikakati mizuri lazima liwe na fedha; na fedha hiyo sisi ndiyo tunaotakiwa tulipe kodi ili tuweze kuliendesha Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuishukuru bajeti imepiga hatua kubwa, ukiangalia kwenye suala la mikopo, mikopo yetu ni himilivu na tunavyokwenda kila siku bado mapato yetu yanaendelea kupanda. Niwape siri Watanzania, ni mtu mmoja ambaye ana uwezo wa kutunza bajeti vizuri, ni mama. Mama siku zote ana uwezo mkubwa wa kutunza bajeti na hili wanaume hawana ubishi nalo, wanajua, hata wao muda wanapoishiwa mifukoni mwao huwa wanasema vipi huko, hali ikoje…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tauhida, ahsante, kengele ya pili.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLONS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Angeline Mabula, jiandae Mheshimiwa Nusrat, jiandae Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, nianze kwa kumshukuru Mungu kwa fursa ambayo nimeipata tena leo kuwa sehemu ya wachangiaji katika bajeti kuu ya Serikali pamoja na hii ya mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze moja kwa moja kwa kuunga mkono hoja kama zilivyowasilishwa japokuwa kutakuwa na machache ambayo nitayazungumzia. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameweza kuendelea na uwekezaji mkubwa katika miradi ya kimkakati, miradi ambayo inakwenda kuongeza pato la Taifa katika kila eneo ambalo uwekezaji huu umefanyika. Nipongeze pia katika vipaumbele ambavyo alivyoweka mojawapo katika taarifa walizozitoa hapa ni kuimarisha uwezo wa uzalishaji wa viwandani na utoaji pia wa huduma ambazo ni bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha uwezo wa uzalishaji wa viwandani, kumewekwa msukumo mkubwa katika suala zima la ukamilishaji wa miradi ipo na ambayo ile inaendelea na tunaiona kwa mfano Bwawa la Mwalimu Nyerere limeshafikia asilimia zaidi ya 95. Kwa hiyo, hiyo moja hapa likikamilika tunaimani umeme unakwenda kusambaa maeneo yote na mpaka sasa hivi upande wa *REA* wamefanya kazi nzuri mno, *almost* vijiji vyote lakini kuna maeneo mengine kuna changamoto kubwa kutokana tu na wakandarasi waliopewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaelekea kwenye uchaguzi, moja ya eneo ambalo linaweza kutuangusha kama hatutaangalia ni upande wa *REA* vijijini na vitongojini hasa kwa wakandarasi ambao wamepewa maeneo, na ukizingatia kanda

ya ziwa kule kazi haziendi vizuri zinasuasua, tungeomba sana hili liangaliwe ili kuweza kusogeza hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima la tozo hasa kwenye maeneo ya uvuvi, nampongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyofanya katika kuwawezesha wavuvi wa Ziwa Victoria lakini pia hata kule bahari kuu kwa maana ya Bahari ya Hindi. Ametoa vitendea kazi vizuri na vingi ambavyo vinawafanya waende kufanya kazi yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto inayokuja, tozo ni nyingi sana kiasi kwamba wanashindwa namna bora ya kuweza kuendelea. Kuna tozo ya asilimia mbili ya mazao ya samaki ambayo ilikuwepo na mwaka 2021 tozo ile ilifutwa na ilifutwa baada ya wavuvi kuandamana kuja kuonana na Kamati ya Bunge na tozo ile ikaondolewa lakini leo tozo ile imerudi; na tozo ile kama hatukuangalia inakwenda kutupeleka kubaya kwa sababu tozo ile pia ilifilisi wavuvi wengi, ikafanya wengi waachane na biashara, viwanda vingi vya samaki vilifungwa kwa kukosa rasilimali, sasa leo tena tunairudisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeomba sana Serikali, changamoto tuliyoipata wakati ule 2021mpaka tozo ikafutwa sidhani kama imepata muamala wa kuweza kuendelea kuirudisha tena, ningeomba sana Serikali iangalie. Lakini naipongeza kwa kushusha tozo ile waliyokuwa wameanza kutoza kwenye mazao ya samaki kutoka shilingi 10 ilipanda mpaka 100 sasa hivi wamepunguza wameenda kwenye 50, nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tozo ya kusafirisha mabondo nayo imeshuka kutoka 3,500 kwa kilo mpaka 2,800 kwa mabichi mabondo, makavu yameshuka kutoka 2,500 mpaka shilingi 2,000 kwa hiyo, hiyo nayo imesaidia. Changamoto ipo katika suala zima la usafirishaji wa mabondo hayo, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu wakati anatoa hotuba yake alizungumzia habari ya kutumia pesa za Kitanzania kwa maana ya shilingi lakini upande huu bado wameacha kutoza kwa dola kwamba wanatoza kwenye mabondo mabichi dola 3.7 ilikuwa dola 2.7 sasa inakuwa dola 3, makavu ilikuwa dola 3.3 sasa inakuwa dola 3.5. Hii inawafanya

wavuvi waendelee kuyumba katika suala zima, ni kipi wanatakiwa kutozwa na ukiangalia wanatozwa zaidi ya 15 ambazo zipo pale, ningeomba sana tozo hii iangaliwe ili kuweza kuona jinsi gani tunaenda kuwasaidia wavuvi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nirudi kwenye gesi, kwa kweli suala la gesi ile huduma bado tunahangaika kuhamasisha halafu leo hatujawa na maeneo mengi ya kufunga ile mifumo, wataalamu wapo wachache na tunahimiza habari ya kuwa na *clean energy* kama askofu alivyosema. Leo hii tukiwapandishia tunataka pia kurudi nyuma suala ambalo Mheshimiwa Rais amekuwa *champion* wa mambo ya *clean energy* na Taifa na *globally* wanaufahamu. Sasa kwa nini tunataka kurudi nyuma? Tungeomba sana, bado uhamasishaji unaendelea na hata magari ya Serikali yenyewe bado hayajafungwa, waliofungiwa ni wachache, huduma bado vituo ni vichache, leo tunawapandishia. Ningeomba sana hilo lisiwepo kwa sababu linatupeleka nyuma na kuturudisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nipongeze Serikali kwa masuala ya *zero rate* katika suala zima la wauzaji dhahabu wanaouza kwenye benki kuu, tuna imani watakuwa wengi na utoroshaji utapungua, kwa hiyo tunaipongeza. Lakini pia pamoja na wale wanaouza dhahabu katika vile viwanda vya uchakataji, tutakwenda kuimarisha viwanda vyetu, tutakwenda kuongeza ajira. Kwa suala hilo kwa kweli naipongeza Serikali kwa sababu ni mambo ambayo yalikuwa na changamoto, watu wanatorosha dhahabu kwa sabau ya kukwepa kodi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mabula kengele ya pili ahsante.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kengele ya kwanza?

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru naomba tu nisisitize kuna mchango wangu nimepeleka kwa maandishi kuhusiana na namna ya kuingiza

vyanzo vingine vya ukuzaji wa uchumi kwa kutumia sekta ya nyumba pamoja na milki ni sekta ambayo imesahaulika na inaweza ikatuongezea pato kubwa la Taifa, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Nusrat Hanje, Mheshimiwa Mafuwe, Mheshimiwa Asya Sharif Omar.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti kuu ya Serikali Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza kwa kujikumbusha na kutukumbusha wote kuhusiana na *4R's* za Mheshimiwa Rais, *reconciliation, rebuilding, resilience* na *reforms.* Kwa maana ya Mheshimiwa Rais wakati anaingia madarakani alitangaza muelekeo wa uongozi wake katika miaka yake atakayokaa madarakani na akazitambulisha *4R's* hizo akimaanisha mageuzi, ustamilifu na kujenga upya Taifa letu, kwa maana ya hizo *4R's*.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitajikita katika *reforms*. Naipongeza sana Serikali na Wizara ya Mipango na Uwekezaji, Wizara ya Fedha na Serikali kwa ujumla. Wamejitahidi sana kuonesha nia na dira ya Mheshimiwa Rais kuhusiana na *reforms,* upande wa *reforms* tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna masuala kadhaa. Ukipitia *Finance Bill* unaweza kuona namna ambavyo mtazamo wa Mheshimiwa Rais umeonekana katika *reforms.* Nitataja maeneo ambayo kwa kweli, mimi kama Mbunge na sisi kama Waheshimiwa Wabunge, kuna mambo ambayo tumekuwa tunashauri ambayo sasa hivi kutokana na hii *Finace Bill* iliyoletwa mwaka huu tunaona namna ambavyo Serikali imejaribu ku-*incorporate* kuyaingiza katika *Finace Bill*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, pamoja na kwamba, nimesoma mapendelezo ya Kamati, nimesoma Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na nimesoma Mpango wa Maendeleo wa Wizara ya Mipango na Uwekezaji, lakini nimeenda

moja kwa moja kwenye *Finace Bill* kwa sababu, huku kwingine kote unaweza ukawa umezungumza mambo mengi, lakini kama hujaleta utekelezaji wake kwa kurekebisha na kutunga Sheria, unakuwa tu ulipiga stori. Kwa hiyo, nimeeda moja kwa moja kwenye *bill* na kuna baadhi ya vitu ambavyo vimewekwa na ninaomba nivitaje, kwa maana ni sehemu ya *reform* ambazo mimi naamini lengo lilikuwa ni hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejadili sana kuhusu *sugar industry,* ukipitia *Finace Bill* utaona marekebisho ya Sheria ya sekta ya sukari na wameleta vipengele viwili ambavyo nitavitaja mahususi. Tukipitisha *Finance Bill* hii hapa itakuwa *dealers* na *manufacturers,* wazalishaji na wasambazaji wa sukari, watalazimika kuwatangaza hadharani wasambazaji wa sukari na mawakala wao kila Mkoa. Kila Mkoa tutakuwa tunajua, kama ambavyo watu wa Cocacola wanatangaza kila Mkoa nani ni msambazaji wao pale kwenye Mkoa husika kwa hiyo, watu wa sukari pia, watakuwa wanalazimika kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, wazalishaji na wasambazaji wa sukari nchini watakuwa wanalazimika kutangaza hadharani gharama ya uzalishaji. Vipengele hivi ni kwenye kutatua tatizo la *monopoly* katika sekta ya sukari, naona tukipitisha *Finance Bill* hii, kwenye kipendele hiki ni sehemu ya *amendment* ambazo ninaamini ni *reforms* ambazo Mheshimiwa Rais amekuwa akizizungumza. Hilo ni eneo moja wapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sehemu nyingine ambayo mimi, kama Mbunge ambaye nimekuwa nikizungumza masuala ya *value chain* kwenye sekta ya madini, Serikali imeleta *amendment* kwenye Sheria ya Madini na inatutaka kabla ya kutoa madini nje, asilimia 20 kila mtu ambaye anashiriki katika mnyororo wa thamani wa madini, asilimia 20 lazima ichakatwe ndani ya nchi, *smelting, refining* na *trading* ni lazima, imeletwa kwenye Sheria. Yani, hivi nikisema imeletwa kwenye Sheria, maana yake ni utekelezaji wake unaanza kuuona, tofauti na tukiongea bila kuona kwenye *Finance Bill. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napongeza kwenye hili. Ni sehemu mojawapo ya *reform,* lakini mimi pia, kama Mbunge ambaye nawakilisha kundi la vijana, nimeona Serikali imeweka kwamba, italeta *venture capital fund* (Mfuko wa mitaji). Lengo la mfuko wa mitaji ni kutoa mitaji kwa biashara ndogo ndogo, *startup* na *SME's*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili naliomba kwa dhati kabisa litekelezwe. Yani Serikali watekeleze hili kwa sababu ni jambo zuri. Litasaidia vijana kuongeza ubunifu na kuweza kuanzisha biashara zao ndogo ndogo kwa sababu wanatoa mitaji kwa kupitia *e-key* na *e-key* ipo kwenye *Finance Bill*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nimekuwa nikizungumza kuhusiana na *digital services tax* na ukisoma Hotuba ya Wizara na Mpango unaona namna ambavyo Serikali inajaribu kupambana kutafuta vyanzo vipya vya mapato. Nimepitia sana na kuna namna unaona sehemu nyingine inaleta mushkeli, lakini unaona wanapambana kutafuta vyanzo vya mapato kwa sababu, wanajaribu kufuata ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kuongeza wigo wa walipakodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona leo katika Sheria ya *Finance Bill* wameweka *content creation capital gain tax*. Kwa hiyo, hii inaonesha kwamba, wanasikiliza maoni ya Waheshimiwa Wabunge wakati mwingine, lakini nikipata nafasi mbele nitaendelea kushauri ni kitu gani zaidi cha kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, wameleta kipengele ambacho kinahusu *online data services.* Lengo pia, ni kulinda taarifa binafsi za watu, lakini pia, wameweka *tax* kwa hiyo, Serikali itaendelea kupata kodi kwenye upande huo, lakini ningependa katika Sheria waweke tafsiri ya watoa maudhui mitandaoni *(digital content creators)* ni akina nani, ili tuone urahisi wakati tunaendelea kuchakata. Tuone kwamba, watu wanaelewa tunawazungumzia akinanani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sehemu moja ambayo hatujafanya vizuri, ni lazima tuseme. Kwanza, ninaunga mkono

kuweka shilingi 382 kwenye *compressed natural gas* na ninaomba ieleweke kitu hiki kimoja, kwanza mtambue kwamba, lengo siyo kuumiza mtu yeyote, lengo ni kuongeza wigo wa walipakodi na kuongeza kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kilo moja ya gesi inauzwa shilingi 1,550 tukiongeza shilingi 382 inakuwa ni shilingi 1,932 tu kwa kilo moja ya gesi, ambayo ni gharama ndogo sana ukilinganisha na *diesel* na *petrol.* Mimi ni mwanamazingira, hiki kitu ni kitu ambacho naona ni sahihi kwa sababu, hizi fedha Waheshimiwa Wabunge mkumbuke zinaenda kwenye *road fund*. Sisi wote hapa, akikaa Mheshimiwa Waziri anayezungumza masuala ya barabara wote humu ndani tunainuka. Hii fedha inaenda *road fund* na inawezekana ikaonekana kwamba, kwa sababu bado hili suala la *natural gas* ni changa, tukaona kwamba, tumewahi sana ku-*tax,* lakini ni vizuri tukaanza kujipanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, mimi nimepitia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na nimeona wale watu wamejinga na ninakwambia *very soon* tutaona *impact* ya hiki kitu. Waheshimiwa Wabunge, nawaomba tafadhari tupitishe hii kwa nia njema ila *at the same time* Wizara ya Fedha ninaomba muachane na tozo ya asilimia mbili kwa wakulima wa hii nchi. *On the other side* tuwapitishie hii shilingi 382, ili tuendelee ku-*tax* huku na tuendelee kujipanga kwenye *natural gas* na asilimia mbili ya wakulima, lakini tafadhali naomba muwaache wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi. Hao mnaowataja ndiyo watu wanaoenda kutupigia kura, maana yake ni vitu vingine mpaka tuambiane kwenye *camera*. Huyu mkulima mnaeenda kumtoza hii asilimia mbili, niwakumbushe, hiki kitu tulipitisha Mwaka 2021 tukakileta kwenye *miscellaneous* hapa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba muachane na hii biashara, hamtoboi. Achaneni na biashara ya wakulima asilimia mbili...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe. Mheshimiwa Asya Sharif Omar na Mheshimiwa Margaret Sitta, mjiandae.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mezani. Kwanza kabisa nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote, mnafanya kazi nzuri pamoja na Naibu Mawaziri, lakini mahususi ni Mheshimiwa Nyongo, kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kila mara tunaposhauri hapa anatusikiliza na anafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikishauri mara kadhaa kwamba, tunaomba Serikali iwe na mpango wa kuanzia miaka 50, miaka 100 na kuendelea. Mheshimiwa Rais amelipokea hili na kesho nina swali linalohusu ombi hilo, nitaliondoa kwa sababu, tayari Mheshimiwa Rais ameshajibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza Profesa kwa Hotuba yake nzuri, unaona kabisa hii imeandikwa na Profesa. Nampongeza sana, lakini ninawaomba, ninafahamu Wizara hii, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji Waziri wake ni nani. Ninafahamu vizuri sana, lakini ninaomba mapema kabisa mnapoanza ofisi hii, Mheshimiwa Nyongo na Mheshimiwa Waziri, mjue hili eneo ni Wizara nyeti sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri hata wakati wa kujadili hii Wizara ingejadiliwa peke yake. Ikae peke yake, tupate muda wa kuijadili peke yake, wawe na nguvu, ili isionekane kazi ya Wizara ya Mipango ni ku-*compile* taarifa za Wizara nyingine. Tunatakiwa tuwape nguvu, wawe na uwezo wa kupanga mipango yetu na iheshimiwe na Mawaziri wote. Hili ni muhimu sana, vinginevyo watakuwa na kazi ya ku-*compile* mipango ya Waheshimiwa Mawaziri na hawatakuwa na nguvu ya kuweza kuwa-*question,* kuwasimamia na ku-*reject* mipango ambayo haiko kwenye utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kuwa na vitu endelevu, mpango ukianza mwaka huu undelee kwa kipindi cha miaka 50 na kuendelea. Pia, nashauri kwamba, Wizara hii inatakiwa iwe na watumishi wasio wa kawaida kwenye *routine activity*. Tutafute *team*, mwaka jana nilishauri hapa ikiwenzekana tuwe na *intellectual team*, wakae vijana watulivu wenye uwezo mkubwa, wajifungie kwa utulivu waweze kupanga mipango ya nchi yetu. Tukiamua kuichukulia Wizara hii kama Wizara nyingine, tutakuwa hatujamsaidia Mheshimiwa Rais na lengo lake la kuanzisha Wizara hii ili tuwe na mipango ya Taifa inayotekelezeka litakuwa haijatimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu namna ambavyo kuna *routine activity*, siku hizi ni bahati mbaya sana hata wakuu wa taasisi akichaguliwa akikaa siku mbili/tatu anaanza kuwaza Ubunge na siasa. Tupate watu ambao ni *free from politics,* ambao watasimama, watalipwa vizuri, waweze kusaidia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwigulu, Waziri wa Fedha, tumekuwa na changamoto ya fedha kutokwenda, lakini nasema hebu tutoke kwenye *routine activity* za kutafuta kodi kila mahali, eneo lilelile. Viko vyanzo vipya, mimi nakutajia vyanzo vipya hapa ukavitafute, ukaviboreshe, lakini mwisho wa siku naomba zile fedha zilizopangwa kwenye Bajeti ya Kilimo zipewe kipaumbele. Fedha za umwagiliaji, ile shilingi trilioni 1.2 iliyopangwa kwenye Wizara ya Kilimo iende na mimi nilimuahidi Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwamba, nitamsaidia kudai hii pesa. Kwa nini nasema hii pesa iende?

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 65 ya Watanzania wamejiajiri kwenye kilimo. Kwa hiyo, ukipeleka pesa kwenye kilimo, umwagiliaji utakuwepo na watu watalima, kwa maana hiyo tutaongeza uchumi. *Formula* ya kukuza uchumi ni kuongeza *productivity* na *productivity* inapatikana kwa Watanzania walio wengi kwenye eneo la kilimo. Sasa pesa unazipata wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekushauri hapa mara kadhaa kuhusiana na *remittance*, nchi nyingi kama Comoro, Nigeria,

South Africa na Egypt wanafanya vizuri kwenye eneo hili. Mbona sisi kwetu haweki kipaumbele?

Mheshimiwa Naibu Spika, kila tunapozungumza hapa mnarudi kwenye mambo yale yale, soda, bia, sijui vinywaji gani. Tunazungumza nendeni kwenye *remittance,* nchi nyingine wanapata fedha nyingi, lakini Mheshimiwa Deo Ndejembi ana kazi ya kufanya hapa kutafuta ajira kwa Watanzania huko nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ukienda nchi nyingine, ukishuka pale Dubai Mall ukiangalia wale walinzi wanaolinda pale na wanaotoa huduma ni wenzetu, wanaongea Kiswahili, lakini siyo Watanzania. Sasa sisi tunashindwa nini kwenda ku-*capture* soko na kupeleka watu wetu huko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikia nchi jirani hapa imepeleka wauguzi nje ya nchi na tunaambiwa kuna nchi nyingi duniani, yuko mchangiaji mmoja alitaja hapa, ambazo zinahitaji watumishi. Sasa Wizara inayohusika na ajira wahakikishe wanaenda huko nje ya nchi kutafuta masoko, ili vijana wetu waende kuajiriwa, ili tuweze kupata fedha nyingi zinazotoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, liko jambo lingine hapa kuhusu hewa ya ukaa. Haya yote ni maeneo ambayo Serikali inatakiwa kuchangamka tutoke kwenye mambo ya kukimbizana na wananchi na wafanyabiashara wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hewa ya ukaa hii ni dili duniani na watu wanapata fedha nyingi. Sasa sisi hapa kwetu Tanzania, eneo ambalo lina sifa ya kuingia mkataba ni hekta milioni 45. Waziri wa Mazingira, Mheshimiwa Selemani, yuko pale anaona na anafahamu jambo hili, lakini eneo ambalo tumeingia mkataba ni hekta milioni 1.8 tu, eneo lingine lote ambalo ni asilimia 00.1. Sasa tunashindwa nini ku-*capture* hizi pesa? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe, kengele ya pili hiyo.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba sana Serikali itusaidie, lakini pia kwenye...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe, kengele ya pili.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Asya Sharif Omar. Mheshimiwa Sitta na Mheshimiwa Ally Kassinge, mjiandae.

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na afya njema, leo nimeweza kusimama katika Bunge letu hili Tukufu. Binafsi nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Serikali ya Mwaka 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumpongeza Rais wetu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pia, nampongeza Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Hassan Mwinyi, kwa namna wanavyoendelea kuwaletea maendeleo ya kiuchumi wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naanza mchango wangu kwenye bajeti hii kwa kumuomba Waziri wa Fedha, kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu na Naibu Waziri wa Fedha kwa kumuwezesha Waziri wetu wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, ili kupata fedha, kwa ajili ya kuwalipa wazabuni kuweza kutekeleza miradi ya maji kwa wakati. Tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan. Sisi wanawake na wanawake wenzetu wa vipato vya chini na vya kati tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa ile adhma yake ya kumtua mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni dhahiri na ni ukweli na kila mtu anafahamu; Mheshimiwa Dkt. Mama Samia amedhamiria kumtua mama ndoo kichwani, ili aweze kufanya shughuli zake za

kujiletea maendeleo. Ni imani yangu Wizara ya fedha italizingatia hilo la kuiwezesha Wizara hii ya maji, ili wakandarasi watimize wajibu wao ikiwemo kutekeleza miradi hii ya kupatikana maji safi na salama kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine utajikita kwenye masuala ya udhalilishaji wa kijinsia. Kama tunavyofahamu, hivi karibuni tumeshuhudia au tumesikia mauaji ya watoto wetu wenye ulemavu (ualbino). Jambo hili limetusikitisha sana, hasa sisi akinamama. Kitendo hiki hakikubaliki na ni cha kukemewa kwa nguvu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, Serikali yetu Tukufu iweze kuwachukulia hatua za kisheria wale wote waliohusika na vitendo hivyo vya kinyama. Tunalaani vikali na tunasema tutakuwa mstari wa mbele kuendelea kupambana na majanga haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusogeza vituo vya afya karibu na sisi. Vituo hivi vimetusaidia sana kupata huduma hii ya mama na mtoto na vimetusaidia kujifungua katika mazingira safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna asiyejua mambo anayoyafanya Mheshimiwa Dkt. Samia, ni makubwa katika nchi yetu. Tutaendelea kumuunga mkono na kumsemea mazuri ambayo anayafanya na ambao hawaoni na hawataki kazi kwao, lakini sisi hapa tunasema 2025 ni Mheshimiwa Dkt. Mama Samia na Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha hoja. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Margaret Sitta. Mheshimiwa Ally Kassinge na Mheshimiwa Eliadory Felix, mjiandae.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyopo mezani.

Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai wa kuwa Bungeni wakati huu. Pia, nawashukuru sana Wapiga Kura wa Urambo na Wananchi wote wa Urambo kwa kweli, wananipa ushirikiano mkubwa. Nawashukuru sana na pia, ninaishukuru familia yangu kwa ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina kila sababu ya kuishukuru Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia kwa kazi kubwa inayoifanya. Kama vile sisi Urambo tuna miradi mikubwa ya Maji ya *Lake Victoria*, umeme, barabara na mengi ambayo naishukuru sana Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Mipango, wote wanafanya kazi kubwa wakisaidiana na Makatibu Wakuu. Kwa kweli, suala la kupata fedha siyo mchezo. Hongereni wote mlioko katika Wizara hizi mbili, za Mipango na Fedha, kwa kazi kubwa mnayoifanya ya kutaka kuiinua nchi yetu kiuchumi. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kikao hiki au tuseme hoja hii iliyoko Mezani lengo lake kubwa ni kuona jinsi gani ambavyo nchi yetu inaendelea kiuchumi. Kwa msingi huo na mimi pia, ninaangalia, je, Wilaya yetu ya Urambo au Jimbo la Urambo linaendeleaje kiuchumi? Ni mambo gani ambayo yanaweza kutusaidia na sisi, kama Wilaya au Jimbo la Urambo, tukachangia katika uchumi wa nchi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ninaloona mimi ambalo ninaiomba Serikali itusaidie, ili na sisi tutoe mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu, ni Mradi wa Maji ya *Lake Victoria*. Watu wa Urambo wakishapata maji watatulia na kufanya kazi nyingine ambazo zitawasaidia kuendelea kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni Mradi Mkubwa wa Kituo cha Kupozea Umeme cha Uhuru. Naishukuru sana Serikali imefanya kazi kubwa na imefikia hatua kubwa, lakini ombi letu sisi ni kwamba, kile kituo cha kupozea umeme kikamilike, ili watu

waweze kufanya kazi zao; wanaouza juisi, wanaosaga unga na kadhalika. Umeme siyo kwa ajili ya kuona tu, lakini pia, ni kujiendeleza kiuchumi. Kwa hiyo, tutashukuru sana kama mradi wetu wa kituo cha kupozea umeme utakamilika haraka kwa kadiri itakavyowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi, kama Wananchi wa Urambo, zao letu kubwa tunalolitegemea ni tumbaku. Tunaishukuru Serikali kwa kutupa ruzuku hata kwenye mazao mengine, lakini ombi letu kubwa, hasa kwa upande wa zao la tumbaku, ni mbolea iwe imefika kabla ya Mwezi wa Nane. Kwa hiyo, ni matarajio yetu kwamba, kwa sasahivi mbolea iko njiani, karibu ifike kwenye maeneo ambayo tunahitaji mbolea kwa sababu, karibu tutaanza kuandaa mabedi ambayo ndiyo tunapanda mbegu za tumbaku. Kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali mbolea ifike kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, wakati huohuo tunaiomba Serikali katika kutoa mbolea ya ruzuku, basi itusogezee vituo, ili wananchi wasiende kuifuata mbali. Kwa sababu, kuna wakati mwingine wanakwenda kule wanakuta mbolea imekwisha inabidi walale, lakini wakiwasogezea karibu maana yake ni kwamba, wakulima watakwenda kununua mbolea na kurudi nyumbani kwao bila kupata usumbufu wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakati huo huo katika kuuza tumbaku zipo kampuni ambazo zinalipa vizuri sana na tunazipongeza, zipo kampuni zinazonunua tumbaku zinalipa vizuri na kwa wakati. Nichukue nafasi hii kuiomba Serikali kutusaidia kwa kampuni zile ambazo karibu miaka mitatu sasa hawajawalipa wakulima tunaomba watusaidie jinsi ya kubana hizi kampuni ambazo hazijalipa wakulima ziwalipe wakulima ili nao wajiendeleze katika njia nyingine za kujiendeleza kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo niwaombe Serikali kwa niaba ya Wananchi wa Urambo kwamba zao letu lingine pamoja na tumbaku zao letu lingine ni asali kwa kufuga nyuki. Nimekuwa nikisimama hapa Bungeni kuiomba Wizara ya Maliasili

na Utalii lakini sasa naiomba Serikali kwa ujumla iangalie jinsi ambavyo inaweza kutusaidia sisi hasa kwa upande wa wakulima wanaotegemea kufuga nyuki kwa kuweka mizinga yao ndani ya pori.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi hiyo niiombe bado Serikali iangalie uwezekano pamoja na kuishukuru Serikali kwa kutupa Hifadhi ya Mto Ugalla lakini bado tunaiomba, Wananchi wa Urambo tumegewe eneo hasa kata zile zinazohusika zipate eneo la kuweka mizinga yao kama walivyozoea. Habla haijawa Hifadhi ya Mto Ugalla wananchi walizoea kufuga nyuki, wanaweka mizinga yao, wanapakua asali wanauza lakini walipokuja kubadilisha sasa kufanya Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla imekuwa vigumu wananchi kupeleka mizinga yao na kuweka mule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado narudia kuiomba Serikali tunaombe tukatiwe eneo katika pori lile la Hifadhi ya Mto Ugalla ili na sisi tuweke mizinga yetu tuendelee kuuza asali kama njia mojawapo ya kuijiendeleza kiuchumi. Pia ninaiomba Serikali pia kwamba wanapoangalia upanuzi wa barabara watuangalie na sisi, barabara inayotoka Usongelani kwenda Tutuo kwenda Sikonge ili ijiunge na barabara kubwa zinazokwenda Mkoa wa Mbeya na Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo nichukue nafasi hii...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sitta ahsante kengele ya pili.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mheshimiwa Eliadory Felix, jiandae Mheshimiwa Agnes Marwa.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi hii nikielekea kuchangia Mpango na Bajeti

ya 2024/2025. Awali ya yote nimshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye sisi Wana-Kilwa tulipopata majanga ya mafuriko mwanzoni mwa mwezi Mei mwaka huu Mheshimiwa Rais akatoa maelekezo juhudi za haraka zichukuliwe ili kuweza kurudisha miundombinu katika hali yake ya kawaida. Kwa hiyo kwa upekee wake nimshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru Mheshimiwa Bashungwa ambaye alikuwepo uwandani kwa kipindi chote mpaka hali imetengamaa. Vilevile kwa upekee wake nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye Kitengo cha Maafa cha Serikali ndiyo kipo chini yake na kwa kweli alitupa ushirikiano wa kutosha na tumepata misaada ambayo angalau imekidhi haja kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa upekee nimshukuru Mheshimiwa Waziri Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu Mheshimiwa Jenista. Nishukuru Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Lindi na Mheshimiwa *RC* Lindi Mheshimiwa Zainab Telack, nimshukuru Mheshimiwa *DC* wa Kilwa, Mheshimiwa Nyundo na Kamati yake ya Usalama ambayo kwa kweli walikuwa bega kwa bega kipindi chote cha majanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru Halmashauri yangu ya Wilaya ya Kilwa chini ya Mkurugenzi wetu, dada yetu Hanan Bafagih ambaye kwa kweli alishirikiana vizuri na wananchi na msaada ambao ameweza kuutoa kupitia halmashauri yetu. Mheshimiwa Rais aliungwa mkono katika juhudi hizi na taasisi mbalimbali za ndani na za nje ya nchi. Kwa hiyo wale wote ambao wameunga mkono katika kusaidia kupunguza majanga ya maafa haya tunawashukuru na hapa nitawataja kwa uchache wakiwakilisha wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Taasisi ya *Blue Springs*, Kampuni ya *Bin Shomari Tanzania Limited* iliyopo hapa Tanzania lakini kwa upekee wake Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Tingi Mheshimiwa Rajab Ngatanda ambaye yeye ndiyo alikuwa

anaratibu pamoja na taasisi hizi ili kuona kwamba misaada ya kibinadamu inawafikia wananchi wetu waliyopata mafuriko.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hao Waheshimiwa Madiwani wetu katika kata zote ambazo zote ambazo majanga haya yalitokea nitumie fursa hii kutoa shukrani zao ikiwemo: Mheshimiwa Chijinga wa Kata ya Masoko; Mheshimiwa Kinjokwile wa Kata ya Kikole; Mheshimiwa Matajiri wa Kata ya Mandawa; Mheshimiwa Rukia Jamadar, Viti Maalumu; pamoja na Mheshimiwa Fatuma Kindamba au Mama Mpulu naye ni Diwani wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Taasisi za Kidini nazo hazikuwa nyuma katika kutakua changamoto zilizotokana na majanga haya ikiwemo BAKWATA, Kanisa la *AICC*-Kilwa, Kanisa la *PFCT* Kilwa pamoja na taasisi zetu ikiwemo *NMB* Kilwa, *TRA* Kilwa, *MSD* pia na watu binafsi walikuwa mstari wa mbele. Tunatoa shukrani kwa wote ikiwemo Umoja wa Wafanyabiashara wa Masoko pale Kilwa Masoko. Watu binafsi kwa upekee wake ambao walitupa ushauri na hususan mimi binafsi nilipata ushauri ni kutoka kwa mtangulizi wangu wa nafasi hii Mwakilishi wa Jimbo la Kilwa kusini Mheshimiwa Seleman Bungala alinipa ushauri wa karibu sana katika kuona kwamba tunaendea vipi utatuzi wa changamoto hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizi nianze mchango wangu katika bajeti hii. Kwanza kwa kutoa rai Serikalini kuwa na mipango ambayo haileti madhara kwa wananchi wetu. Wakati tunapitisha mpango wa tatu wa maendeleo hapa tulipitisha uboreshaji na upanuzi wa viwanja vya ndege 12 vikiwemo viwanja viwili vya Kilwa Masoko pamoja na Kiwanja cha Ndege cha Nachingwea. Kwa masikitiko niseme tu kwamba viwanja hivi wananchi wetu bado hawajapewa fidia baada ya tathmini ambayo imeshafanyika kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Nachingwea mpaka sasa hivi wananchi 113 bado hawajalipwa shilingi bilioni 3.4. Tunasubiri nini, Serikali inasubiri nini kutekeleza kitu ambacho walipanga wenyewe wakati tunapitisha Mpango wa Tatu wa

Maendeleo? Wananchi wangu wa Kilwa Masoko wapatao 447 wana-*cover* vitongoji viwili mpaka leo bado hawajalipwa fidia yao kiasi cha shilingi bilioni sita na ushee hivi. Serikali inasubiri nini kulipa fidia kwa wananchi wetu hawa ambao wameendelea kupata madhara baada ya tathmini kufanyika?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni zaidi ya mwaka sasa wamekumbwa na mafuriko, hawana makazi Serikali inasubiri nini? Suala hili mimi hapa Bungeni nimelizunguma hapa Bungeni nimelizungumza mara kadhaa. Nimelizungumza katika swali la msingi namba 18 Mkutano Kumi na Tatu, Kikao cha Pili tarehe (01 Novemba, 2023). Nimelizungumza katika swali la nyongeza namba 30 Mkutano wa Kumi na Nne, Kikao cha Pili (tarehe 31 Januari), 2024. Nimelizungumza wakati nachangia Hotuba ya Waziri Mkuu Mkutano huu wa Kumi na Tano, Kikao cha Tatu (tarehe 04 Aprili). Pia nimelizungumzia kama swali la msingi, niliuliza swali la msingi namba 76 Mkutano wa Kumi na Tano, Kikao cha Sita, tarehe 15 Aprili mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini majibu ya Serikali ni kwamba tukipata fedha tutalipa. Niseme tu kwamba Wananchi wa Kilwa wataona mpango huu una maana na bajeti hii ina maana endapo Serikali itakuja kutoa tamko hapa haraka iwezekanavyo wananchi hawa wa Kilwa, Nachingwea na viwanja vingine vilivyofanyiwa tathmini wakalipwa haraka iwezekanavyo iili kuondoa adha inayoendelea. Tarehe 15 Februari mwaka huu timu ya wajumbe kadhaa ikiwemo wawakilishi wa wahanga wa tathmini hii, walikuja hapa wakakutana na uongozi, wakakutana na Serikali ikiwemo Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Fedha mwenyewe Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na akawaahidi kwamba atawalipa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia bajeti hii nakumbusha wananchi wangu hawa waweze kulipwa fidia yao ili mambo mengine yaendelee...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Ally. Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix...

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Jiandae Mheshimiwa Agnes Marwa, jiandae Mheshimiwa Khadija Shabaan Taya.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi nitoe mchango wangu kwenye Bajeti Kuu. Niwapongeze watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango kwa kazi kubwa na njema wanayoifanya. Niishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miradi mingi ambayo inatekelezwa Mkoani kwetu Kigoma na katika Wilaya yangu ya Buhigwe ambayo ipo kwenye hatua mbalimbali. Nasema ahsante na hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mchango wangu katika Bajeti hii Kuu utajikita kwanza kwenye uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta ambayo ni alizeti ambayo inalimwa sana sana katika Mkoa wa Singida, Simiyu, Shinyanga na Dodoma. Zao la pili ni chikichi ambayo Mungu alituzawadia Kigoma, makao makuu na sehemu ambayo ni ukombozi kwa kilimo cha chikichi ni Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazao haya ni mazao ya kimkakati. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa miaka miwili mitatu nimeshuhudia kwa macho juhudi kubwa ambavyo amehamasisha kilimo cha chikichi Kigoma na kilimo cha alizeti Singida. Amezindua na amewatembelea wakulima. Mazao haya ni ukombozi kwa Taifa letu yanaweza yakaokoa fedha nyingi za kigeni ambazo tunazitumia kwenda kununua mafuta ya kula. Mazao haya (alizeti na chikichi) yakiwekewa msisimko, yakawekewa ruzuku, yakawekewa nguvu kubwa ya kisekta na Wizara ya Kilimo ikahamasisha, mazao haya yanaweza yakaokoa fedha nyingi tunazozitumia kuagiza mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri unajionesha kwenye Taarifa ya Wizara ya Fedha. Mwaka 2019 uzalishaji wa zao la alizeti kwa mwaka ilikuwa ni tani laki 561,297 lakini baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhamashisha kwa mwaka jana 2023 alizeti iliyozalishwa hapa nchini ilikuwa ni tani 1,103,298. Kwa zao la chikichi kwa mwaka 2019 chikichi iliyokuwa ikizalishwa ilikuwa ni tani 42,176 baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhamasisha na kuja mara kwa mara katika Mkoa wetu wa Kigoma uzalishaji umeongezeka kutoka tani 42,000 hadi kufikia tani 62,125 kwa mwaka jana (2023).

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kuzunguma ni nini? Hatuna sababu yoyote ile ya kutumia fedha za kigeni ambazo zinaendelea kuwa chache kuagiza mafuta nje ya nchi wakati sisi Mungu ametupa ardhi nzuri, yenye rotuba na uwezo wa kuzalisha mazao haya. Tunaweza tukazalisha na hiyo *gap* ya mafuta ikafutika. Kinachohitajika ni juhudi, tunahitaji huduma bora za kilimo ziongezwe katika mikoa hiyo inayozalisha alizeti na chikichi na mazao haya yapewe ruzuku maalumu kwa ajili ya kuongeza uzalishaji bora. Zaidi tafiti ziendelee zaidi kupata mbegu bora ambazo zinaweza zikazalisha mafuta mengi ili kuokoa fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili mazao ya biashara kahawa na chai. Tuna mikoa 16 inayolima kahawa na mikoa ambayo inalima kahawa vilevile inalima na chai. Mazao haya ni muhimu kwa nchi yetu kwa sababu ndiyo yanayotupatia mchango mkubwa, ndiyo yanayotupatia na kutuingizia fedha nyingi za kigeni lakini mazao haya mawili uzalishaji wake unashuka. Ukiangalia kwa mwaka 2019 kahawa iliyozalishwa nchini na kuuzwa nje ya nchi ilikuwa ni tani 68,147 lakini kwa mwaka jana (2023) tani zilizozalishwa na kuuzwa nchi za nje ni tani 62,917.

Mheshimiwa Naibu Spika, chai kwa mwaka 2019 chai iliyozalishwa na kuuzwa nje ya nchi ilikuwa ni tani 37,193 lakini kwa mwaka jana (2023) ni tani 23,775. Mazao haya ya biashara uzalishaji wake unashuka kwa nini? Ni kwa sababu Serikali haijachukua maamuzi ya dhati kwenda kutatua changamoto zinazowakabili wakulima wa chai na kahawa. Tunaomba bajeti hii

ikatatue matatizo ya wakulima wa kahawa na chai ili uzalishaji uongezeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante, kengele ya pili hiyo.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni waliokaa Jukwaa la Spika wageni watatu wa Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga wawekezaji kutoka Austria: Ndugu Wolfgang Rainer Fuchs, karibu; Ndugu Romana Turek; Ndugu Jachina Chuma Kihwelo, karibu. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge: wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Waziri wa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo familia yake kutoka Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 35 wa Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel, Naibu Waziri wa Afya, wanafunzi wa Shule ya Siha leadership kutoka Siha Mkoa wa Kilimanjaro wakiongozwa na Askofu Mafie ambaye ni mlezi wa Mheshimiwa Waziri wa kiroho na mwanae Namnyaki Godwin Mollel, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 22 wa Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Waziri wa Madini kikundi cha *Friends of Mavunde*. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Innocent Kalogeris ndugu yake kutoka Mkoa wa Morogoro Ndugu Mohamed Matokeo. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Noah Saputu Wenyeviti wa Vijiji kutoka Arumeru Mkoa wa Arusha, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 22 wa Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay walimu na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Mkoa wa Manyara.

Wageni 20 wa Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima Makatibu Wenezi kutoka Wilaya ya Singida Mjini.

Mgeni wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe na Bi Joshua R. Mwanyatara.

Wageni 77 wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula na Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Mwanza, viongozi wa Taasisi ya Kumwombea Mheshimiwa Rais na Wasaidizi Wake (TAKURAWA) kutoka Mkoa wa Mwanza, karibuni. *(Makofi)*

Wageni nane wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati Kwaya ya Ebenezer kutoka Kanisa la *AICT* Ndachi, Dodoma. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo: vijana 60 na viongozi watano kutoka Kituo cha Maendeleo na Mtoto na Kijana Kanda ya Kati kutoka Singida, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 34 *Wanautalii Tanzania Organization*, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Mheshimiwa Agnes Marwa, jiandae Mheshimiwa Taya, jiandae Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na mimi kwa kuchangia Wizara hii ya Fedha. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anazifanya katika Taifa hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Rais wa Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi kwa kazi nzuri anazozifanya lakini kuleta mapinduzi makubwa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niende moja kwa moja kwa kuishauri Serikali kuhusiana na masuaa haya ya tozo. Moja kwa moja, naishauri Serikali hili zuio la asilimia mbili kwa wakulima ni jambo ambalo mimi kama Mbunge ningeshauri ni jambo ambalo haliwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa tunatafuta pesa sehemu mbalimbali tukumbuke kwamba hawa wakulima kwanza wanalima kilimo cha shida sana, wanalima kilimo cha gharama za chini sana, lakini pia kwao pesa kidogo ni tatizo sana. Hata kukopesheka benki ni shida, ni majuzi juzi tu Mheshimiwa Rais alisababisha sasa wakulima wameanza kukopesheka na Waziri wetu Mheshimiwa Bashe, lakini bado wakulima wana hali mbaya sana. Kwa hiyo mimi niiombe Wizara hii tozo ya asilimia mbili kwa wakulima wetu iondolewe, siyo jambo zuri.

Mheshimiwa Naibu Spila, pia, hii tozo ya asilimia mbili kwa samaki, jamani tunajua kabisa kwamba wavuvi wa Tanzania, masoko yenyewe hawana, maeneo ya kwenda kuuza hizo samaki kwa gharama ambayo inaweza ikawarudishia fedha ya kutosha hawana, sasa hata hiki kidogo wanachokipata pia tuwanyang'anye? Mimi nadhani kwa kweli tunapaswa kuangalia ni sehemu gani tunaweza tukatafuta hizi fedha lakini kwa hawa wakulima, kwa hawa wauza samaki au hawa wavuvi nadhani hizi tozo ziondolewe, zisirudishwe tena maana wauza samaki, wauza dagaa, wakulima, kwa ujumla maisha yao yanajulikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania bado hatujafikia hatua ya kwamba sasa tumefikia tumepata masoko ya hali ya juu kiasi kwamba wakaingiza fedha za kutosha. Kwa hiyo, ombi langu kwa Serikali ni hilo, kwanza tuondoe hii tozo ya asilimia mbili, tuwaondolee kwanza hao wakulima, tuwaondolee wavuvi lakini tuondoe kwenye samaki ili na sisi sasa tufaidi samaki zetu za Tanzania pia hawa wavuvi wafaidi uvuvi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami pia niendelee kumpongeza Waziri wetu Mheshimiwa Bashe, maamuzi aliyoyafanya ya kuleta sukari wakati ule wa mwezi mtukufu ambao wote tulikuwa tumefunga waislamu na wakristo, mimi nafikiri ni jambo zuri sana,

alitumia maamuzi mazuri sana kama baba, siyo mpaka usubiri uone nyumba inaungua mpaka muende mkakae kikao cha ukoo ndiyo muanze kuamua kwamba tufanye nini. Yeye moja kwa moja akafanya maamuzi na tukapata sukari ambayo kwa kipindi hicho ilikuwa ni adimu sana kwa kweli tunakushukuru sana na tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu maana mfungo wetu ulikuwa mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye suala la wafanyabiashara. Wafanyabiashara wetu wa Tanzania tunatamani sana watoe hizi tozo lakini wanapokuwa wanatoa hizi tozo basi sisi tuwafanye watoe ziwe tozo rafiki zinapokuwa tozo rafiki mimi naamini watatoa, siyo kwamba hawahitaji kutoa isipokuwa tozo zimekuwa nyingi sana zinawazidia, zinapowazidia hapo ndipo inapotokea wengine wanajificha wengine wana maduka ya nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona nchi za wenzetu tunapotoka kwenda nje, tukienda nje wewe mwenyewe utaitoa tu kwa sababu hata yule mfanyabiashara kutokana na mazingira aliyotengenezewa ana uwezo wa kuitoa kutokana na kwamba, kwanza iko chini, ni bei nafuu, lakini ni rafiki. Sasa hivi tukiingia uadui na hao wafanyabiashara linakuwa siyo jambo zuri sana. Mimi naamini kabisa Serikali yetu ina nia nzuri sana ya kukusanya kodi, hata kwenye biblia kodi imeandikwa, kwenye misaafu imeandikwa. Kwa hiyo, hata Mwenyezi Mungu anakubaliana na kodi. Mimi niwaombe sana wafanyabiashara wa Tanzania tukae chini tukubaliane kukaa chini na Serikali yetu, tuongee tuwaambie ni kodi ipi ambayo kwetu ni *reasonable* kwa maana ya sisi tunaweza tuka-*afford* kuitoa ili tuweze kufanya biashara vizuri lakini na Serikali ikusanye kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali tukakae na wafanyabiashara tukae tuangalie hizi tozo tukazipunguze, tuwape tozo nafuu ambazo wanaweza kulipa kila mmoja, kila Mtanzania aweze kulipa kodi ili tusiwe na mivutano huku na huku. Mimi naamini kabisa mpaka sasa hivi mivutano inayoendelea yawezekana baadhi ya wafanyabiashara kuna kodi ambazo

zinawazidia na ndiyo maana wanakuwa wanavutana na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda moja kwa moja kwa kumshukuru na kumpongeza sana Rais wangu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri sana alizozifanya katika Taifa hili la Tanzania. Mkoani kwangu Mara, Mama yetu tunakupongeza sana, tunakuombea sana, Mama yetu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Marwa, ahsante.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Niiombe sana Wizara sasa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Marwa, muda wako umekwisha, ahsante.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Taya, jiandae Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, jiandae Mheshimiwa Taska Mbogo.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kupata fursa ya kuchangia bajeti kuu. Kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na uzima aliotupa, pili naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais, nikupongeze Mheshimiwa Rais, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi zote ambazo umefanya, umeapa kushughulikia watanzania na kweli tunaona nia yako thabiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Mawaziri wake pamoja na watendaji wote kwa kazi nzuri ambazo kusema kweli mnafanya, ambapo mnaleta maendeleo katika nchi yetu na tumeona baadhi ya mifano mizuri ya Mawaziri ambao wanachukua maamuzi magumu sana lakini yote kwa ajili ya

wananchi wao. Kwa hiyo, niipongeze Serikali ya Mama Samia, nipongeze Awamu ya Sita ya Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wetu kipenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu, Wabunge wako hawa wana uchungu, wanazungumza vitu vizuri wanatengeneza hoja nzuri za kupata mapato, tunatengeneza sheria humu ndani, tunatengeneza bajeti na tunapitisha bajeti. Hii yote ni kwa sababu ya wananchi ambao ndiyo wametupa kibali cha kuja kwenye nyumba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema sisi ni wenye bahati sana, tuna bahati kwa sababu tumepata kuweza kufanya kazi, kazi ambayo ukiifanya vizuri utasifiwa na binadamu, lakini ukiifanya vizuri zaidi utaweza kupata thawabu kwa Mwenyezi Mungu ambaye ametuumba sisi wanadamu wake. Hilo ni jukumu kubwa sana lakini ni bahati kubwa sana na kuwa mtumishi wa umma na wewe una-*responsibility the same* kama Mbunge ambaye yupo kwa ajili ya wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo, hawa Wabunge wako wanapitisha, Bunge hili linapitisha bajeti, bajeti kwa ajili ya wananchi. Tunawapa thamani au tunawapa watu ambao wanaenda kusimamia hizi hela zifanye kazi. Juzi tumesikia pale Arusha kwa Kaka yangu *RC* Makonda ambaye pia anafanya kazi nzuri, tumesikia kuna pesa ambazo zinaenda lakini hazifanyiwi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi yetu sasa hapa ni nini, tunajukumu gani? Jukumu letu tushauri Serikali kitengo kile cha tathmini au *monitoring and evaluation* peke yake chini ya Waziri Mkuu bado naona hakitoshi, kwa sababu hiki kitengo hakina pesa ya kutosha. Kwa nini sasa tusitengeneze sheria ya kutengeneza mamlaka kamili ambayo hiyo mamlaka itaweza kuijisimamia kuanzia juu mpaka kwenye Halmashauri huku chini tukaweza kuzisimamia vizuri pesa zetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kuna *CAG* ambaye anakuja baada tatizo limeshatokea. Kwa nini tusitengeneze

mfumo mzuri, tunafahamu pesa kiasi gani imeengia Dodoma Mjini, ipo kwa malengo gani, kwa hayo malengo sasa tuone hiyo pesa inaenda kweli kwenye hilo eneo na je, zile *criteria* ambazo zimewekwa na wataalam wetu zinafuatwa? Unaenda hospitali katika vituo vya afya wamejenga *tiles* kabla ya kile kituo hakijatumika, *tiles* zimeanza kuonesha unyevu unyevu wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoteza zile pesa ambazo tunazipitisha hapa lakini tunawalipisha kodi wananchi wetu. Tuangalie namna gani ya kuleta mamlaka rasmi ya kuhakikisha hizi pesa ambazo tunazitenga hapa zinaenda kufanya kazi inayotakiwa kufanya na zinaenda kusimamiwa inavyotakiwa kusimamiwa. Hili ni jukumu letu Wabunge tuhakikishe tunaleta hii sheria na tuitetee kwa nguvu yetu yote ili mamlaka rasmi ya tathmini na ufuatiliaji iweze kuundwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sijaishukuru Serikali ya Mama Samia. Juzi nizumezungumza masuala ya mtoto na mauaji ya watu wenye ualbino, Serikali imesikia, Mama Samia ametoa pole, Mheshimiwa Waziri Mkuu kaja hapa na mikakati mizuri ya kuondoa shida ya watu wenye ulemavu. Nasema ahsante sana Mama Samia, Nasema ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini naomba kusisitiza mambo ambayo tumeyapanga, mikakati ambayo tumeipanga tuende kutekeleza na twende kuwakumbusha wananchi wetu huku chini kulinda watu wenye ualbino, lakini kuhakikisha tunaondoa zile hali za watu kuwa na uwoga. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa kengele yako ya pili.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Ahsante Mheshimiwa, Daah! muda mfupi sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, jiandae Mheshimiwa Taska Mbogo, jiandae Mheshimiwa Nicodemas Maganga.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii na mimi niweze kuchangia

kwenye hoja ambayo iko mezani bajeti ya Wizara ya Fedha pamoja na Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri na kwa jinsi anavyoongoza Taifa hili kwa ufanisi na umahiri mkubwa. Pia, nichukue nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wetu wawili hapa Dkt. Mwigulu Nchemba na Prof. Kitila, Naibu Mawaziri wake Mheshimiwa Chande na Mheshimiwa Nyongo kwa kazi nzuri ambayo wanafanya na hotuba inayoeleweka, bila kusahau watendaji kwenye hizi Wizara mbili kuanzia Katibu Mkuu na watumishi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii ambayo tumeona mafanikio makubwa kwenye utekelezaji wa mambo mengi hapa nchini. Miundombinu inaendelea kutekelezwa, usafirishaji, *SGR* sasa hivi imefikia 96 *percent* kutoka Dar es Salaam mpaka Makutupora, lakini pia Bwawa la Mwalimu Nyerere ujenzi wake umefikia asilimia 98 na sasa hivi umeshatupa kwenye Grid ya Taifa *Megawatts 470*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia bajeti ya kilimo ikipanda sasa hivi ni zaidi ya trilioni na uzalishaji wa chakula umevuka asilimia 124, pia matumizi ya mbegu bora na mbolea umeongezeka na maeneo ya umwagiliaji yameongezeka imefikia hekta 730,000. Haya mafanikio siyo kidogo, kwa hiyo niseme moja kwa moja kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo mafanikio nina machache ya kusema hasa kuhusu barabara. Barabara zimejengwa sana, sasa hivi tumefikia kilometa 181,600 lakini mafanikio haya sioni kama yamekuwa na *impact* kwenye Jimbo langu. Kwa hiyo, niseme wazi kwa Waziri wa Fedha na Mipango kwamba waweke mpango wananchi kule Arumeru Mashariki wa-*feel* mafanikio haya ya ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi kule Arumeru Mashariki wako milimani na wanafanya kilimo cha viazi na *carrot,* baada ya kuvuna mazo yao wanashindwa kuyapeleka sokoni

kwa sababu ya shida ya barabara. Najua kwamba kuna mradi unaotekelezwa Nyanda za Juu Kusini wa *Agri-connect*. Sasa niishauri Serikali ifikirie namna gani italeta mradi kama ule kule Nyanda za Juu Kaskazini ili wananchi wanaolima milimani waweze kupeleka mazao yao sokoni. Mradi wa Nyanda za Juu Kusini unatekelezwa na wadau wetu wa maendeleo, sasa nasi tujiongeze kidogo tuanzishe huo mpango tuutekeleze *locally*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 13 Novemba, 2020 Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dkt. Magufuli kwenye hotuba yake ya kuzindua Bunge alisema dira yake ya utekelezaji wa majukumu yake ingeongozwa na Ilani ya Utekelezaji, Mpango lakini pia na ahadi. Tarehe 22 Aprili, 2021, Rais wa Awamu ya Sita hapa ndani akasema mambo hayo hayo akarudia na akasema ndiyo urithi ambao amechukua, lakini sasa nimekuwa nasema hapa ahadi ahadi toka mwaka 2020 mpaka leo hakuna ahadi hata moja kule Jimboni imetekelezwa. Niishauri Serikali itekeleze zile ahadi kwa sababu ndiyo urithi ambao Serikali ya Awamu ya Sita ilichukua kwa Serikali ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanikiwa sana kwenye kilimo lakini kule kwetu Arumeru Mashariki tuna Mashamba ya Kili Flora ambayo yamechukuliwa na Serikali baada ya mwekezaji kuyatelekeza. Niishauri, lile shamba la Kili Flora ambalo liko chini ya Wizara ya Fedha lifanywe kama mradi wa *BBT,* kuna vijana wengi hawana kazi kule Jimboni waweze kuingia kwenye hilo shamba wajikimu na kujiendeleza kimaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia kengele ya kwanza sitaki unipigie tena ya pili, nakushukuru kwa nafasi hii naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Mbogo, jiandae Mheshimiwa Maganga, jiandae Mheshimiwa Shigongo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuchangia bajeti ya Serikali. Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai tupo hapa tunachangia bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nianze na shukrani nyingi kwa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambayo ameifanya kwa watanzania hususan kwenye mambo mbalimbali ya elimu, afya, miundombinu pia mpaka juzi amedhihirisha upendo wake kwa watanzania kwa kuunda Tume ya Haki Jinai ambayo inamwezesha kila mtanzania kupata haki yake. Mheshimiwa Rais anahitaji pongezi kwa sababu ni kwa mara ya kwanza nchini kwetu Tanzania inaundwa Tume ya Haki Jinai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo ningependa kujielekeza kwenye suala la miundombinu nchini Tanzania. Sisi wananchi wa Mkoa wa Katavi tunaishukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ujenzi wa barabara kutoka Tabora kuja Mpanda kwa kiwango cha lami. Pamoja na hizo shukrani tunamshukuru pia kwa ujenzi wa Bandari ya Karema kule kwenye Ziwa Tanganyika ambayo itawezesha meli kutoka Congo kuja kutua kwenye Bandari ya Karema na pia itaweza kubeba mzigo kutoka Karema - Mpanda hadi kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo ninayo maombi kwa Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Maombi yetu ni suala la kufungua Mkoa wa Katavi, pamoja na hizo barabara ya Tabora - Mpanda, bado Mkoa wetu wa Katavi haujafunguka kwenda kwenye Mikoa mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba tupewe barabara ya kutoka Kibaoni kuja Stalike ambayo ina kilometa 71, lakini kwa sasa hivi ujenzi wa barabara hiyo umesimama kwa sababu ya ukosefu wa pesa, hata Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi alikwenda pale akawatoa wafanyakazi ambao ni wabovu lakini bado barabara hiyo imesimama. Ombi langu kwa Serikali itupe pesa barabara yenye kilometa 71 Kibaoni - Stalike iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la pili, tunaomba tupewe barabara kutoka Kibaoni – Usevya - Majimoto mpaka Inyonga, Inyonga pale wanakuja kuungana na barabara ya lami ambayo

inatoka Tabora-Mpanda. Barabara hii ni muhimu kwa sababu inabeba mazao yanayotoka kwenye Bonde la Mwamapuri, bonde hilo lina kilometa takribani hekta 18,000 ambazo zinatoa mpunga unaolisha nchi jirani za Congo, Rwanda, Burundi lakini na nchini kwetu Tanzania. Hivyo basi, upo umuhimu wa kuijenga barabara hii ya kutoka Kibaoni – Usevya - Majimoto mpaka Inyonga kwa kiwango cha lami, barabara yenye urefu wa kilometa 165 ili tuweze kufanya biashara vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo ombi la barabara nyingine ya kutoka pale Mpanda Mjini kwenda mpaka maeneo ya Karema ambako tumejenga Bandari ambayo iligharimu takribani bilioni 47, fedha za kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara kutoka Bandarini kuja Mpanda Mjini haina lami, ni barabara ya vumbi. Hivyo basi, azma ya kujenga Bandari inaweza isifanikiwe vizuri kama hatutaweza kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Ombi langu; ninaiomba Serikali ijenge barabara hii ambayo ina takribani kilometa 125.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lingine ni la ujenzi wa barabara ya kutoka pale Vikonge – Luhafwe mpaka Uvinza ili Mkoa wetu wa Katavi uweze kuungana na Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la tatu ni la barabara ya kutoka pale Mpanda Mjini kupitia Ugala ambako kuna daraja linajengwa. Hivyo tunaomba fedha za daraja hilo ili liweze kukamilika na barabara hiyo iweze kutoka Mpanda – Ugala – Kaliua – Kahama mpaka Nyakanazi ili tuweze kupata wafanyabiashara kutoka Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maombi ya barabara hizo sisi tunapenda kusema ahsante kwa Serikali ya Awamu ya Sita kwa fedha ambazo zimekuja kwenye Mkoa wetu huu wa Katavi kwa kipindi cha miaka mitatu. Ombi letu ni kukamilishiwa huu usafiri ili Mkoa wetu wa Katavi uweze kufunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lingine ambalo ningeweza kuliomba kwa Serikali ya Awamu ya Sita, tungeomba pia tukamilishiwe baadhi ya miradi. Kwa mfano tunao mradi wa kuvuta maji kutoka Ziwa Tanganyika kuja pale Mpanda Mjini. Mradi huo wa kuvuta maji kutoka Ziwa Tanganyika kuja Mpanda Mjini utaweza kunufaisha mikoa ya jirani kama Mkoa wa Rukwa pamoja na vitongoji ambavyo vinapita pembeni mwa mradi huo. Mradi huo ni mkubwa, bado haujaanza, lakini uko kwenye kufanyiwa tathmini. Tungeomba, ili kutatua tatizo la maji kwenye Mji wa Mpanda Mjini tunahitaji maji yavutwe kutoka Ziwa Tanganyika. Sasa hivi maji yaliyopo hayatoshelezi kwa sababu wananchi wameongezeka. Kama sensa ilivyopita mwaka jana, Mji wa Mpanda umekua na wananchi wameongezeka, hivyo mahitaji ya maji ni makubwa, yaliyopo hayatoshelezi na yanatoka kwa mgao kwa siku moja moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ombi lingine ambalo ningeiomba Serikali ya Awamu ya Sita tunaomba ule Mradi wa Umwagiliaji wa Mwamapuli ambao uko kwenye Halmashauri ya Mpimbwe utekelezwe. Mradi huu ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye aliwaahidi wananchi wa Mwamapuli…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbogo….

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maganga ameomba kuchangia na hayupo, Mheshimiwa Eric Shigongo, jiandae Mheshimiwa Vita Kawawa. Wote hawapo. Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge, Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Olesendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii. Vilevile nikushukuru pia wewe mwenyewe binafsi kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuchangia mpango wa maendeleo pamoja na bajeti ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kukushukuru na kukupongeza kwa kuendelea kuliwakilisha Jimbo lako la Ilala vizuri, kwa sababu unakumbuka mpaka jana ndipo suluhu ya wafanyabiashara wa Kariakoo ilipopatikana. Mchango wako ulikuwa mkubwa sana wa kuifanya Serikali kuelewa tatizo lililokuwa linawakabili wafanyabiashara wa Kariakoo; ninakupongeza sana kwa jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitatumia nafasi hii kumshukuru sana Dkt. Tulia Ackson kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kuliongoza na kuliwakilisha Bunge hili, pamoja na Spika wa Bunge la Afrika Mashariki wakati wa msiba wa ndugu yetu Dkt. Mulozi Sedoyeka ambao ulitokea katika Mkoa wetu wa Manyara. Dkt. Tulia Ackson aliongoza Wabunge wengi sana kuja kutushika mkono. Ukiacha hilo aliweza kuja na chifu wa kabila lao kutoka Mbeya na kutuletea rambirambi ya kumshika mkono mume wa marehemu, Mheshimiwa Profesa Eliamani Sedoyeka. Kitendo hiki kwa kweli kilitufariji watu wa Manyara; na ninapenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Wabunge wa Mkoa wa Manyara kumshukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu niwaombe wananchi wa Mbeya waendelee kumsaidia sana na kumuunga mkono Mheshimiwa Spika ambaye ni lulu ya nchi yetu kwa nafasi yake kama Spika lakini ni zawadi waliyoitoa kwa dunia kama Rais wa Mabunge ya Dunia. Hakika Mbeya imetutendea haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nataka nijielekeze kuchangia baadhi ya mambo madogo sana na machache ya jimbo langu ambayo yanatokana na masuala ya uharibifu wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kabla sijafanya hivyo nataka nitumie nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Profesa Kitila Mkumbo na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu pamoja na Naibu Mawaziri wao wawili pamoja na watendaji wa Wizara hizo kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kutuandalia taarifa hii ambayo ni nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tumeathirika kutokana na janga la EL-Nino ambapo miundombinu ya barabara zetu imeharibika. Hata hivyo, niseme bayana kabisa kwamba Jimbo letu la Simanjiro limeathirika kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo kata nyingi ambazo kwa sasa barabara zake hazipitiki. Pamoja na jitihada za Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kutuwezesha kujenga tuta la Msitu wa Tembo na miundombinu katika Kata za Msitu wa Tembo, Kata ya Ngorika, Loiborsoit, Ruvu Remit pamoja na Darala la Gunge, ukanda wote huo umeathirika kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa bonde la maji linalohudumia maeneo ya Kata ya Shambalai, Endiamutu, Mererani na Kata ya Naisinyai ni vizuri wakashirikiana na Serikali pamoja na TAMISEMI na Wizara zinazohusika na wadau wanaohusika kuhakikisha kwamba maji yanarudi kwenye mkondo wake, kwa sababu maji yameacha mkondo wake na kuleta athari kubwa kwenye mazao ya wakulima pamoja na athari kubwa ya kuharibu miundombinu katika ukanda huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ilani ya uchaguzi tunazo barabara kubwa tatu ambazo ilani ya uchaguzi ilitoa ahadi kwamba ingeweza kutekeleza. Hii ni Barabara ya kutoka Arusha – Losinyai – Komolo – Terrat – Naberera – Namalulu – Orkesumet kulekea Ndido kwenda Kiteto kuja hadi Kongwa. Hii ni barabara ndefu ambayo ilipangiwa fedha kupitia *EPC + Finance*. Ni rai yangu kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na wahusika wote wahakikishe hiyo fedha inapatikana ili hiyo barabara ya *EPC + Finance* iweze kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilani ya uchaguzi pia iliahidi kujenga barabara inayotoka Mererani – Landanai – Langai kuja Orkesumet na barabara inayotoka Babati kupitia Galapo kuja kuingia Kimotorok – Roiborsiret – Narakawo kuja Sukuro na kuelekea makao makuu ya Wilaya ya Simajiro na *branch* inayokwenda mpaka Kiteto.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hakuna barabara kati ya hizi ambayo imepata fedha ya kujengwa. Rai yangu kwa Wizara ya Fedha na kwa Waziri Mkuu wa nchi yetu, ni vizuri barabara hizi zinapogawanywa, na hasa barabara za lami kila eneo lionje na kupata kilometa chache. Kama bado mnao urasimu mkubwa kwenye barabara hii ya *EPC + Finance* au hamjakamilisha uwezo wa kuwezesha barabara hii kuanza, ni ushauri wangu kwa Serikali yangu sikivu ya CCM, anzeni hata barabara moja kwa kutupatia kilometa hata 20 kwa mwaka inayoweza kutusaidia ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Jimbo la Simanjiro na majimbo ya wafugaji nao wanapata barabara nzuri ambazo wanazihitaji katika kusafirisha mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kuishauri Serikali yangu sikivu ya CCM kuangalia suala zima la kuwezesha ujenzi wa shule za bweni katika maeneo ambayo jiografia inaweka mazingira magumu zaidi. Shule zetu za Kata tumejenga kwa nguvu za wananchi; hata hivyo ni dhahiri kwamba umbali kutoka kijiji kimoja kwenda kijiji kingine ni mkubwa zaidi. Kwa hiyo, nilitaka kuiomba Serikali ione uwezekano wa kuwa na *affirmative plan, affirmative action* katika maeneo ambayo ni magumu ili Serikali iweze kutenga fedha za ujenzi wa mabweni kwa sababu wananchi wamejenga zile *hostel* na hivyo Serikali iunge mkono jitihada za wananchi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kuendelea kuikumbusha Serikali yetu sikivu ya CCM, leo sina haja ya kugusia masuala ya mapori, tumekwishakuzungumza na Waziri na tuliomba Serikali itoe kauli katika suala linalohusiana na mapori tengefu, na kwa hiyo leo sina sababu ya kugusia hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie suala ambalo Mheshimiwa Rais amelizungumzia juzi alipokuwa anazungumza na baadhi ya watumishi aliowateua katika ile Tume ya Haki Jinai, kuhusiana na malengo ya Serikali yetu au misingi tunayoitaka katika nchi yetu; kwamba ni kuongoza katika misingi ya uhuru, haki, usawa na kuthamini misingi ya utu. Nitumie nafasi hii kumwomba Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuingilia kati suala la Ngorongoro. Tulikwishakubaliana kuwa

wananchi wa Ngorongoro waliopo tayari kuhama waweze kuhama kwa hiari yao kama ambavyo Serikali ilitoa kauli; na tunaunga mkono jitihada za wale waliohama kwa hiari yao. Hili ni vizuri likaeleweka bayana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka niseme wazi. Ni vizuri Serikali ikaondoa vikwazo vinavyokwaza maisha ya wananchi wa Ngorongoro. Pale ambapo unayo shule kama ya *Ngorongoro Girls* iliyopo katika Kata ya Lailole ambayo miundombinu yake ya maji inahitaji *pump* ya *ku-pump* maji kutoka mtoni kuleta pale shuleni na fedha zipo, ziko pia fedha za kujenga bweni katika Shule hiyo ya *Ngorongoro Girls* lakini mpaka leo fedha hizo hazijatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya shule zimebomoka vyoo, kuta za madarasa na hakuna fedha zinazopelekwa kwenye maeneo hayo. Ni dhahiri kwamba vitendo hivi vinakwenda kinyume na misingi tuliyojiwekea kama Taifa (Misingi ya haki, utu na kuthamini kwa kweli heshima na utu wa watu wanaoishi katika maeneo hayo).

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai yangu kuishauri Serikali ya CCM ikiongozwa na mtendaji anayeongoza kwa niaba ya Rais, Waziri Mkuu wasaidie kuwezesha miundombinu hiyo ili kuondoa fedheha na aibu ya kuonekana kwamba Serikali ya CCM inawawekea vikwazo vya kimaisha wananchi wake kwa kushinikiza watu kuondoka Ngorongoro. Itaharibu zoezi zima la watu kuondoka kwa hiari. Ni vizuri watu waondoke kwa hiari, wasiwekewe vikwazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna vyoo vimebomoka vijengwe, kama kuna madarasa yaliyobomoka yajengwe, *pump* ya maji msilazimishe watoto wa kike wa *Ngorongoro Girls* waende kilometa nzima kwenda kuchota maji kwenye mto ambao wanyama nao pia wanakwenda pale na hivyo kuhatarisha maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Olesendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama muda umekwisha naunga mkono bajeti na mpango wa maendeleo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma, jiandae Mheshimiwa Shigongo.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, nimepigiwa simu mara kadha wa kadha na wananchi ambao ni wafanyabiashara wa Mkoa wa Mbeya na mahala pengine. Nimepigiwa simu, wanalalamika kwa namna ambavyo Serikali imeeleza kuhusu faini ya milioni 15, na kama siyo faini ya milioni 15 basi mtu anakwenda kutumikia kifungo jela.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara wetu hawa walio wengi mitaji yao inaweza ikawa milioni nne, milioni tano. Hata hivyo, kwa sababu na wao wanajua na kutambua kwamba wanatakiwa kutoa kodi, risiti na yote hiyo ni kwa ajili ya manufaa ya ujenzi wa Taifa letu hili la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi sana hizi mashine za *EFD* zinaweza zika-*stuck*. Hizo mashine zikigoma wanapeleka kwa wahusika ili wawarekebishie na hivyo waweze kutoa risiti. Utakuta mtoaji ama mtengenezaji wa mashine hiyo anakuwa hayupo yuko safarini anasema atarudi baada ya siku mbili au siku tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu hizo fedha wanakuwa wamekopa. Kwa namna ambavyo wanataka maisha yaweze kuendelea akimpatia mfanyabiashara risiti ya mkono ili kama anakaa maeneo ya jirani aje kuchukua risiti ya *EFD* pale ambapo *EFD machine* itakapokuwa imetengemaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapa katikati mfanyabiashara huyu akipatikana na tatizo la kutotoa risiti inakuwa ni tatizo kubwa sana. Sasa hapa kama anachukuliwa hatua ya faini ya milioni 15, mtaji wake ni milioni nne au milioni tano hizo fedha atazitoa wapi? Wananchi wetu wa Tanzania tunawajua kabisa jinsi ambavyo wanajihangaisha kwenye shughuli hizi za biashara. Tutalundika wafanyabiashara wangapi kwenye magereza?

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Serikali yetu ya Awamu ya Sita ya mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Rais wetu, ni mama mwenye hekima, ana busara, upendo na ana mapenzi mema kwa Watanzania wake. Hapendi kuona Watanzania wanapata matatizo au wanaingia kwenye shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninadhani na ninatumaini kwamba inawezekana hili jambo ni Wizara ya Mipango na Wizara ya Fedha ndio ambao wamelileta. Mheshimiwa Rais mama yetu kipenzi ambaye anawapenda sana Watanzania wake na wao wanampenda sana tunaomba aliangalie na kulirekebisha jambo hili la faini za milioni 15 ili wafanyabiashara hawa waweze kuendelea kufanya biashara zao kama jinsi ambavyo walikuwa wakiendelea kufanya kama nchi ilivyotengemaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wetu hawa walio wengi ni wazalendo. Maana tunajua kwamba nchi bila kodi hakuna kinachoendelea. Nchi bila kodi hatujengi hospitali, barabara, hatufanyi chochote, na kwenye masuala ya elimu kutakuwa kumelala.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri sana Serikali iliangalie kwa umakini suala hili la faini ya milioni 15 ama kifungo cha kwenda jela kulingana na sisi wenyewe Watanzania tulivyo. Wafanyabiashara wa Mkoa wa Mbeya na baadhi ya mikoa mingine; na bahati mbaya sana nilipita hata Dar es salaam; maduka yamefungwa. Nilishangaa kwa nini nikaambiwa ni kwa sababu ya hii faini na kwamba hawataweza kulipa faini hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashauri kwamba, Serikali mkae vizuri sana na hawa wafanyabiashara kurekebisha utaratibu ili kufikia mwafaka na kazi ziweze kwenda. Pia, ukizingatia kwa mfano pale Dar es salaam nchi nyingi zilifika ili kununua mizigo ili wapeleke kwenye nchi zao, wanabaki wameduaa na wanashangaa. Hii siyo sawa, kiasi kwamba tunaweza tukapoteza mapato mengi ambayo yangetakiwa kuingia Serikalini kutokana na mauzo yale, lakini sasa ilishindikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana na ninamwomba sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, mama yetu huyu ambaye ana hofu ya Mungu; siamini sana kwamba hili jambo alikuwa analielewa vizuri; ninamwomba sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, mama yetu tunayemwombea kila siku kwa Mwenyezi Mungu namna anavyoiongoza nchi yake hii ya Tanzania na Serikali yake yote kwa ujumla kuwaangalia hawa wafanyabiashara wa Taifa hili la Tanzania hususani wafanyabiashara wa Mkoa wa Mbeya ambao hawana mitaji mikubwa kiasi hicho. Tunamshukuru sana kwa sababu tunaamini atakwenda kufanya vizuri vile ambavyo anawajua Watanzania wake, kwamba ni masikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Wageni 86 umoja wa wanawake waimbaji wa Injili (CHAMWITA) wakiongozwa na Genesi Mwakifedha na Flora Mbasha kutoka sehemu mbalimbali nchini Tanzania. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni 20 wa Mheshimiwa Malembeka ambao wanatoka katika taasisi ya kumuombea Rais pamoja na wasaidizi wake. Karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Shigongo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa nafasi ya

kusimama katika Bunge hili Tukufu ili niweze kutoa mchango wangu kwa Taifa langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Buchosa. Sisi Buchosa tunahitaji barabara yetu ya lami kutoka Sengerema hadi Nyehunge ijengwe. Kwa hiyo, nimetumwa na wananchi wangu, kwamba fedha zitengwe ili barabara ile iweze kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nataka nizungumzie Taifa langu Tanzania. naipenda sana nchi hii, na ushahidi wa uoendo wangu kwa nchi yangu ni uamuzi wangu wa kumwita binti yangu jina Tanzania. Kwa hiyo hayapo mashaka ya kwamba mimi ninaipenda nchi yangu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii, nisome *data* kidogo tu, kwa utalii Duniani ni ya pili, Afrika ni ya kwanza kwa utalii. Nchi yangu kwa makaa ya mawe ni ya 50 Duniani, kwa gesi asilia ni ya 82 Duniani, Tanzania kwa dhahabu ni ya 22 Duniani, kwa *Helium* ni ya kwanza Duniani, kwa almasi ni ya 10 Duniani, kwa *Tanzanite* ni ya kwanza Duniani, Tanzania ni nchi tajiri sana hatuwezi kuwa maskini hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaposikia mtu anasema nchi yangu maskini, mimi huwa sikubaliani na hilo jambo na sitaki watoto wa nchi hii waelewe nchi yao ni masikini, nchi yetu ni tajiri sana hatuwezi kuwa jinsi tulivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Venezuela ni nchi ya kwanza Duniani kwa mafuta, inafuatiwa na Saudi Arabia, na Urusi ya tatu lakini Venezuela ni nchi masikini sana kuliko Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka nimpongeze Rais wetu wa Awamu ya Sita kwa uamuzi wake wa kutumia sekta za uchumi kuongeza Pato la Taifa huo ni uamuzi wa Rais wetu kwamba amaeamua sekta zote za uchumi zichangie Pato la Taifa ili pato la Mtanzania mmoja mmoja liweze kuongezeka nampongeza sana Mheshimiwa Rais na Waheshimiwa Wabunge na Mawaziri niwaombe tumuunge mkono Rais ili sekta zote za

uchumi ziweze kuchangia Pato la Taifa hatuwezi kuwa maskini kwa utajri tulionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze Wabunge na nikupongeze wewe kwa uamuzi wa Bunge hili kupambana kubadilisha Sheria ya Manunuzi. Tumebadilisha Sheria ya Manunuzi na Kanuni zimebadilika kwamba kuanzia tarehe 01, Julai hakuna mgeni yeyoye anayefanya biashara ya bilioni 50 kushuka chini kwenye nchi hii. Tumefanya jambo jema sana tutakumbukwa kwa uamuzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumedalili Sheria ya Manunuzi, Kanuni lakini kuna jambo moja tusipolifanya mabadiliko haya hayatatusaidia chochote. Benki zetu za Tanzania zibadilishe mtazamo wake kwa wafanyabishara wazawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi hii benki zetu hazitaki kuwekeza sana kwenye biashara zinataka kuwekeza kwenye mikopo ya wafanyakazi na watu wadogowadogo. Hauwezi kutajirika kwa fedha yako mwenyewe kuitoa laki moja kwenda milioni moja ni rahisi. Ila kuitoa bilioni moja mpaka bilioni 100 ni kitu kimoja kigumu sana *you have to use the bank,* lazima tutumie fedha za watu wengine. Kanuni ya utajiri inasema hivi *use other people's money* sasa wenye pesa ni benki, kama benki zetu hazitabadilisha mtazamo wake kuwasaidia wazawa wa nchi hii waweze kuchukua fedha na kufanya biashara mabadiliko haya ya sheria tuliyoyafanya hayatasaidia chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba leo nitoe elimu kidogo, naomba nitoe elimu ndogo tu ya kitu kinachoitwa *triangle of money* ambayo matajiri wote wa nchi hii wanaitumia pembe tatu ya pesa upande mmoja ni A, upande wa pili ni B na upande wa tatu ni C iko chini, naomba nisikilizwe vizuri A ni mtengenezaji wa bidhaa B ni mnunuzi na C hapa chini ni mfanyabiashara. Sasa mfanyabiashara anaingia mkataba na *TFC* kwa kuiuzia labda mbolea, watakubaliana kwamba tutanunua nao mbolea tutalipa kwa siku tisini, mfanyabiashara huyo anaenda kuongea na mtengezaji wa mbolea yuko China au Urusi wanakubaliana atalipa kwa siku 120 anadaiwa kwa siku 120 analipa kwa siku 90.

Matokeo yake hapa ni kwamba kama mbolea ni ya milioni 100 mimi sina milioni 100 nitaenda benki. Benki inatengeneza *back-to-back LC* yaani *back-to-back LC* ni kwamba inaingia mkataba na mnunuzi atalipa kwa siku 90 benki inaingia mkataba na muuzaji wa mbolea atalipa basi 120, maana yake ni nini? Nitalipwa na Serikali siku 90 kabla sijadaiwa na mtengenezaji wa mbolea maana yake hapo ni nini? Unatengeneza pesa bila kutumia pesa lakini benki lazima ikae nyuma yangu kunisaidia, benki zetu haziko tayari kufanya jambo hilo ni waoga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba *CRDB* wamejitahidi lazima niwapongeze na Mheshimiwa Bashe nimpongeze sana amewasaidia sana wafanyabiashara kwenye korosho kule kutumia mfumo huu Mtanzania anafanya biashara ya bilioni 100 anasaidiwa na benki tutumie mfumo huu kuwatajirisha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wamechoka kuwa masikini, mimi mwenyewe nimechoka kuwa masikini. Nataka Watanzania watajirike kwa sheria hii kwa sababu hawana mtaji benki ziwe tayari kufungua *back-to-back LC* kuwasaidia ili huu mfumo wa pembe tatu ya fedha niliousema uweze kusaidia, hauhitaji pesa kupata pesa na hili jambo lazima lieleweke. Kama benki zinaogopa basi Serikali iwe tayari kutoa *government guarantee* kwamba kwenye korosho unahitaji bilioni 300 Serikali itoe karatasi peke yake *government guarantee* kuzipa benki ili ziwakopeshe Watanzania waweze kufanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hilo lieleweke na kama jambo hili likifanyika nakuhakikishia Watanzania watabadilika, tumechoka kuwa maskini lazima jambo hili lifanyike tusaidie tuweze kutoka hapa tulipo. Kwa hiyo, kuendelea kuona wageni wanakuja hapa kila siku wanatajirika sisi tunaendelea kuwa maskini hatutaki na sisi hatutaki kuchukia siku moja tuweze kuwa kama nchi nyingine, tunataka amani ya nchi yetu iendelee kuwepo na Watanzania waendelee kunufaika na nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema hivi mambo manne ya kufanya kuisaidia nchi yangu la kwanza Sekta za Uchumi zichangie Pato la Taifa. Lazima tuhakikishe jambo hili linafanyika kama utalii umechangia Mheshimiwa Rais amecheza sinema mapato yameongezeka kutoka Dola milioni 900 mpaka Dola bilioni tatu ndani ya miaka mitatu iwe hivyo kwenye uvuvi, madini na kilimo nakuhakikishia tukifanya hivi iko siku tutapunguza mikopo tunayokopa, tutapunguza *budget deficit* na kesi ya bajeti inapungua tutatumia fedha zetu kujiletea maendeleo wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni suala zima la Sheria, Sheria zetu tulizonazo ziwe zinatoa fursa kwa Watanzania wazawa kufanikiwa, Sera zetu za Uchumi tuzipitie upya. Inawezekanaje mfanyabiashara wa Kitanzania akafungue duka Zambia? Inawezekanje mfanyabiashara wa Kitanzania akasajiri malori yake Rwanda? Kuna shida mahali fulani hapa ndani lazima tupitie upya *tariff* zetu ziwe za ushindani inawezekanaje ukanunie mashuka Kenya? inawezekanaje ukanunue mashuka Uganda? Kuna nini hapa kwetu ambacho kinakosewa? Tutazame upya sera zetu za Uchumi na sheria zetu ziwe ni zinazoshindana na nchi jirani tunapigwa bao tukiwa tunaona? Haiwezekani tukaendelea namna hiyo kama kweli tuna nia njema ya kuendeleza nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni upendo kati yetu sisi wenyewe Watanzania tupendane, Watanzania tubebane haiwezekani akaja mtu kutoka China akafanikiwa mimi Mtanzania nikabaki chini. Nchi yetu imefika mahali ukitaka kazi mahali fulani unalazimika kumkodisha mzungu wa kukodisha. Wako wazungu wanakaa Serena pale wanalipwa Dola 500 kwa saa, akaonekane mzungu ili wewe Mtanzania upate kazi, naomba Watanzania tupendane tushirikiane sisi kwa sisi ili tuweze kuinuka kwa pamoja katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni *law enforcement*, Sheria tunatunga, tuzisimamie ili kwamba sheria hizi wanaozivunja wapate adhabu inayowastahili. Haiwezekani watu unakusanya fedha zinaliwa watu wanaiba halafu bado hawawezi kidhibitiwa

na sheria zetu. Tuna sheria nzuri sana, tuna Sheria ya Manunuzi nilishaisema, tuna Sheria ya Utakatishaji Fedha, Sheria ya Fedha, Sheria ya TAKUKURU, sheria hizi zote zikisimamiwa sawasawa tutawadhibiti wote wanaoiba fedha zetu kutakakuwa na hofu na woga kwenye fedha za umma hatuwezi kwenda hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma niliwahi kushauri kwamba tutafute utaratibu wa kuwachapa watu wanaoiba fedha za umma. Sasa mimi ninashauri tuongeze idadi ya magereza kwa watu wanaoiba fedha za nchi yetu…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Eric.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Munde Tambwe.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia bajeti iliyopo mbele yetu. Awali ya yote na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunisimamisha mbele ya Bunge lako Tukufu niweze kuchangia bajeti ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya. Hakuna asiyejua wala asiyetambua kazi kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Rais, tunampongeza sana na tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kumpa hekima busara na afya ili aendelee kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha kaka yetu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa bajeti nzuri aliyoileta hapa lakini nimpongeze Waziri wetu wa Mipango kaka yetu Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo na yeye kwa taarifa nzuri ya mipango hakika taarifa imekaa kiprofesa-profesa taarifa ni nzuri sana tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia moja kwa moja kuhusu Tabora, nikienda kwa ujumla kwa Tabora naomba niongee kwa sababu muda ni mchache. Niombe sana Serikali pale Tabora Manispaa tuna kata za ndani na kuna kata za nje, zile kata zetu za nje karibia zote zinazozunguka Manispaa yetu ya Tabora barabara zake ni chakavu ni mbaya zinahitaji kabisa kwa makusudi mazima kuangaliwa kwa upya *at least* ziwe na lami. Kwa sababu pale ni manispaa lakini pia ni mkoa wa siku nyingi sana, wa zamani, hakika ni aibu kubwa kuwa na mkoa kama ule wa miaka mingi ambao mpaka leo baadhi ya kata zake barabara hazipitiki tunaomba Serikali ituangalie kwa jicho la pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tena watu wa TAMISEMI kama wapo hapa watanisikia pale Tabora tuna soko letu zuri tulijengewa na Serikali ya wamachinga, soko lile liko chini kabisa lilipauliwa vibaya wafanyabiashara wote wanafanyia biashara zao nje ya soko. Masika linajaa maji kiangazi jua ni kali, kwa hiyo ndani wametoka kabisa wameliacha. Niombe Serikali itufanyie dharura kuhakikisha tunapata pesa za kujenga soko lile vizuri la wamachinga, Waziri wa TAMISEMI kama yupo hapa ananisikia ninaomba sana mdogo wangu Mheshimiwa Zainab Katimba nimekuona ikiwezekana baada ya Bunge hili tuongozane mimi na wewe kwenda Tabora Manispaa kuangalia soko lile la wamachinga, hali yao ni mbaya wanashindwa kufanya biashara vizuri hawana sehemu nzuri ya kufanyia biashara. Mheshimiwa Rais ametoa fedha amewasaidia sana wamachinga lakini watendaji wetu hawakuwatendea haki. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri nimekuona twende tuongozane Tabora wakati una-*wind up* uniambie ili tukalikague lile soko la wamachinga pale Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana Serikali kwa mabadiliko pia ya *procurement* kuhakikisha wageni wanapata kazi kuanzia bilioni 50 kwenda mbele, hili ni jambo jema la kuwajali Watanzania na Watanzania hakika wameona Serikali yao inavyowajali na kuwasaidia tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongee suala moja la *EFD receipt*, ukifanya biashara yoyote na Serikali au na kampuni yoyote unaambiwa upeleke *invoice* na *EFD machine* ukipeleka ukifika kule unaweza ukalipwa baada ya miezi minne au mitano lakini wakati huo umeshai-*print EFD* kwa hiyo, wewe inabidi ile *EFD* uilipie *VAT, TRA* lakini wewe hujalipwa ile pesa. Niiombe Serikali hatukatai kulipa kodi, maana ni wajibu wa kila mtanzania, lakini sasa *EFD* ipelekwe wakati mimi nataka kulipwa pesa, yaani sasa kesho kutwa unalipwa lete *EFD* ili tukulipe pesa zako. Lakini ukichukua *EFD* kabla sijalipwa, hamtendi haki kwa wafanyabiashara wanabaki na madeni makubwa lakini bila kujua kwamba wamepata pesa, inabidi akakope ili alipe *EFD*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongee sasa Sheria ya Sukari na mimi nichangie kama Wabunge wenzangu walivyochangia. Kwa ujumla niipongeze Serikali kwa kuleta hapa Sheria ya Sukari, niiombe Serikali wakati Waheshimiwa Wabunge wanaipitisha sheria hii ya sukari cha kwanza tumuombe Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, tunaomba wenye viwanda wote wawe na mawakala kwenye mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakala wako Dodoma, Dar es Salaam na Mwanza *imagine* mtu anatoka Tabora ana duka lake la rejareja la sukari apande *bus* aende Mwanza anunue mifuko 10 ailete Tabora akifika Tabora bei ya sukari lazima iwe imepanda. Kwa hiyo, tunaomba kabisa kwenye sheria wahakikishe wenye viwanda wanakuwa na mawakala kwenye mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niombe kwenye sheria hiyo itakapokuwa inatungwa inaletwa hapa Bungeni wawe wametupa bei elekezi ya sukari tupate bei elekezi ya sukari tujue sukari itauzwaje kwenye mikoa yetu lakini pia iwe na bei elekezi ya kununua miwa kwa wauza miwa kama tani ni 70,000 au ni 100,000 basi iwe inaeleweka ili pia kuwalinda wale wakulima wanaouza miwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kushangaza sana unapoona sukari kwenye nchi yetu ni bei kubwa lakini Rwanda sukari iko chini, Malawi sukari iko chini, Zambia sukari iko chini,

unajiuliza tatizo ni nini na sisi tuna viwanda, tuna mashamba ya miwa, Rwanda hawana hata kiwanda lakini sukari iko chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imefika wakati sasa Serikali ijue gharama ya uzalishaji wa sukari kwenye kiwanda kilo moja inazalishwa kwa shilingi ngapi? anaifikisha sokoni kwa shilingi ngapi? kwa nini sukari hii inakuwa bei kubwa Tanzania Malawi bei ndogo, Zambia bei ndogo, Rwanda bei ndogo, tatizo ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana tuiombe Serikali tumuombe Waziri na wataalamu wake watuambie kwa nini sukari Tanzania inakuwa bei kubwa na kwenye sheria waandike labda ni lazima kila baada ya mwaka wabadilishe na kutuonyesha gharama za uzalishaji wa sukari ukoje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la sukari limekuwa kubwa ni lazima sasa tujikite kuhakikisha kwamba tunaenda nalo vizuri lakini pia naunga sana mkono Serikali kuileta sheria hapa Bungeni kwa sababu hatuwezi kuachia tu vitu hivi ambavyo Watanzania wote karibia *almost* asilimia 90 ya Watanzania wanavitumia viwe tu mikononi mwa wafanyabiashara wachache, je, siku yoyote imetokea *market failure*? Mfano imetokea mvua kubwa kama iliyotokea miwa ikawa imebebwa na maji unamwambia sasa ndio nampa kibali kaagize sukari anaagiza sukari unaambiwa kuna vita Gaza meli inazunguka kutoka Brazil, meli inachukua miezi mitatu huku kuna mvua hatuna *stoke* yoyote ya sukari kama Serikali utawaambia nini Watanzania? Watanzania watalaumu tu wakiona sukari 10,000 huwezi kuwaambia eti oooh, nimewapa kibali wafanyabiashara bado sukari haijafika, bado sukari sijui meli imezunguka, lazima Serikali ijitosheleze kwa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenye jukumu la kujua usalama wa chakula wa nchi hii ni Serikali, mwenye jukumu la kujua sukari nyingi au ni ndogo ni Serikali, mwenye jukumu la kujua tuna *stoke* ya kutosha ya sukari ni Serikali. Huwezi kuja Waziri ukatuambia kwamba eti sukari hakuna na mimi nilikuwa sijui wenye viwanda wamefungia sisi hatutakuelewa. Kwa hiyo, hili ni jukumu la Serikali

kuhakikisha linashika mikononi hiki kitu wanaki-*control* si unaona hata kwenye mafuta kuna baki ile ya mafuta wanaleta kwa *procurement* ile lakini kuna mtu ana *control* anajua kwenye baki mafuta yamebakia kiasi gani, nani kachukua mafuta kiasi fulani, nani anauza mafuta kwa bei gani, yaani kila kitu kinakuwa kiko *open* na kuna mtu anajua.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukiwauliza *EWURA* watakuambia kuna mafuta nchini kiasi fulani. *Petrol station* kwa mfano wanayo kiasi fulani na bei ya kuuzia ni hii bei imepanda kwa shilingi hizi kwa nini imepanda bei imeshuka kwa shilingi hizi kwa nini imeshuka. Niombe sana kwenye sukari waige mfumo huo na iwe wazi ili Watanzania wasije wakaingia kwenye janga hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa kilimo kaka yangu Mheshimiwa Hussein Bashe kwa ujasiri wake aliokuwa nao kwa uzalendo mkubwa aliouonyesha na amewaonyesha Watanzania. Siku nyingine sisi Waislam tunaambiwa useme *Alhamdulillah*' kwa kila jambo. Tulivyomuona Mheshimiwa Mpina anafanya yale watu wakasikitika wengine lakini kumbe Mwenyezi Mungu alitaka aonyeshe ukweli wake na ukweli umebainika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, basi kwa kusema hayo naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Gulamali, umerudi.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia kwa siku ya leo. Kwanza nipende kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambayo ameendelea kulifanyia Taifa letu. Tumeona mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere limeongeza *megawatt* za uzalishaji wa umeme wa Taifa, lakini tumeona juzi Treni ya Umeme imeanza kazi kutoka Dar es Salaam kuja Morogoro kwa hatua ya awali. Kwa hiyo, ni mafanikio makubwa sana tunaipongeza Serikali kwa hatua hizi kubwa ambazo zimefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina yangu machache tu ambayo nataka Wizara hii ya Fedha iweze kutusaidia, kwanza Mheshimiwa Waziri umeona kumekuwa na uhaba sana wa dola. dola imekuwa ni changamoto na wewe kama Waziri unapaswa uangalie ni namna gani ambavyo dola hii inatakiwa ipatikane kwa wingi kama ilivyokuwa zamani. Kukosekana kwa Dola kunaleta changamoto kubwa sana hasa kwa wafanyabiashara na hii baadae inaleta athari ya bei ya bidhaa mbalimbali kupanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukienda benki wanakuambia dola wanauza 2620 nenda waambie naomba dola wanakupa kiwango kisichozidi dola 500 au Dola 1000.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mfanyabiashara au wafanyabiashara wanaoweza kuagiza mafuta, kuagiza bidhaa nje ya nchi wanahitaji dola kuanzia labda 100,000 mpaka 1000,000 hawazipati. Lakini wakienda mtaani wanapata Dola, wanaipata dola kwa bei ya juu mpaka 2820, sasa kama mtaani dola zinapatikana huku kwenye mfumo rasmi dola hazipatikani hebu Wizara muangalie namna gani ambayo mtarahisisha upatikanaji wa dola mrahisishe maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maisha ya Watanzania yanakuwa ghali kwa sababu ya ukosekanaji wa dola, sasa Mheshimiwa Waziri na timu yako mtusaidie dola ni changamoto na ni kero kubwa inawezekana ziko changamoto lakini Kenya wamefanyaje wameweza? Kwa nini sisi tushindwe kufanya mbinu ambazo majirani zetu wamefanya na wamefanikiwa ni kweli walikuwa nayo changamoto lakini sasa hivi changomoto hizo tena hawana sisi tuombe Serikali na Wizara mjipange muone ni namna gani ya kuweza kuhakikisha kwamba dola inapatikana na kwa bei ambayo ni katika *rate* ambayo ni *reasonable*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Wizara ya Fedha wanatoa fedha wanatuambia wametoa fedha za miradi ya maendeleo mfano wanatuambia kwenye halmashauri zetu tumepewa fedha za kufanya miradi mbalimbali. Lakini hizo fedha hazitoki sasa tunaziangalia *figure* tu tunazo hela, lakini hela hazitoki kwenda

kwenye miradi, mwezi wa nne hakuna fedha, mwezi wa tano hakuna fedha, mwezi wa sita hakuna fedha miezi mitatu hiyo na mwezi wa sita ukifika mwisho tarehe 30 tunafunga tunaanza mwaka mpya. Kwa hiyo, tena mwaka mpya kuna miezi mingine mitatu mnatulia wa saba, wa nane na wa tisa na ukichukua miezi mitatu ya mwanzo na miezi mitatu hii inakuwa miezi sita maana yake katika halmashauri miezi sita hakuna kazi yoyote inayoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Waziri na timu yako hebu fungulieni hiki kipindi kilichobakia hizo hela zilizopo tunazozisoma ziweze kutoka, kuna watu wanapata tabu. Mheshimiwa Waziri labda hufahamu kuna wazabuni wamefanya kazi pamoja, halmashauri hawapati fedha hawalipwi na halmashauri. Halmashauri inasema fedha tumeambiwa hizi hapa lakini uwezo wa kuzilipa hakuna kibali hamjatoa Mheshimiwa Waziri toeni vibali ili halmashauri ziweze kufanya kazi na wazabuni waweze kulipwa na maisha ya Watanzania yaendelee kuboreka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine Mheshimiwa Waziri wa Fedha nataka nikukumbushe Waziri wa Fedha sisi kule kwetu tuna Barabara ya Choma kuja Ziba kuja Puge inapita Nsimbo na Nkinga hii ni barabara kubwa ambayo kila mwaka tunaahidiwa kujegwa kwa kiwango cha lami, 2015 tuliahidiwa, 2020 imo mpaka kwenye Ilani ya CCM leo ni mwaka wa nne tunakaribia kwenda wa tano hatujapewa fedha za ujenzi wa barabara hii ya lami. Mheshimiwa Waziri wa fedha tumeona unatoa fedha kwenye barabara mbalimbali nchini hii ya kwetu utatoa fedha lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Mheshimiwa Waziri katika majibu yako utuambie maana yake Waziri wa ujenzi anasema mimi sina tatizo Wizara ya Fedha wanatakiwa watoe fedha. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha toa fedha ili barabara hiyo iweze kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami vinginevyo maana yake tutakwenda 2025 sijui tutaenda kuwambia nini tena wananchi, fedha ziko wapi, tunawaambia fedha tunazo, haya leteni mjenge tunawaambiwa Wizara ya Fedha, haiwezekani,

mtatupa wakati mgumu sana kwenye uchaguzi. Niombe sana Mheshimiwa Waziri ujitahidi katika bajeti hii ambayo tumeipitisha au tunaenda kukupitishia kesho uhakikishe fedha za barabara ya lami ya Choma - Ziba - Nkinga - Nsimbo mpaka Puge unatoa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri nadhani utakuwa umenielewa au utasahau? Maana yake najua una mambo mengi sijui jambo gani tukuambie ili ukumbuke kwamba hii barabara inatakiwa itolewe fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzijuzi tulipata matatizo pale ya mabasi na yanaanguka kule maeneo ya Shinyanga wale wagonjwa mmewaleta kule Nkinga na mnatembea vizuri kwenye barabara ya lami mkifika Ziba kuwapeleka Nkinga barabara ni ya vumbi mbaya kwelikweli na ni *rough* mnawapeleka Ndala kule kwa Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla barabara yenyewe mbaya kwelikweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunauliza nyinyi wagonjwa mnawatoa kwenye lami mnawaleta kwenye Hospitali ya barabara ya vumbi si wengine wanakufa njiani hata kabla hawajafika hospitalini halafu inakuja helkopta kutoka Dar es Salaam inakuja kuwachukua wagonjwa kwenye hospitali ya rufaa lakini hospitali ya rufaa haina barabara ya lami. Sasa Mheshimiwa Waziri haujaona umuhimu wa hii barabara kuwekewa lami kweli? Hebu niombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu wako, na timu yenu tunaomba fedha ya barabara ya lami mtupe tumechoka kusubiri kipindi kirefu. Tumeona hata ile Mheshimiwa Waziri pale kwako unaanza utaratibu wa kuweka lami sasa na mimi nafurahi kwa sababu ni *shortcut* ya Ndagu kutokea Singida unaweka lami na sherehe kubwa ilifanyika na mimi naomba mfanye sherehe kubwa pale kwangu Jimboni Manonga Ziba na kwa Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kule Ndala barabara ya lami Mheshimiwa Waziri ni *Serious* maana yake haya mambo tunaona tu kwenye video maeneo mengine na sisi tunapenda mambo kama haya mazuri yafanyike kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nakukaribisha sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba pamoja na Mheshimiwa Chande nakumbuka uliwahi kupiga *push up pale* Ndala na ulipiga *pushup* pale Nsimbo mwaka 2015 na 2020. Sasa 2025 utakuja kupiga *pushup* au utakuja kufanya nini tena? Maana yake unakujaga pale kuomba kura kwa wananchi sasa sijui utakuja? Au hauji safari hii. Maana yake uliowaambia utawajengea lami ni wewe na 2015 ni wewe na 2020 ni wewe, sasa 2025 utakuja na staili gani? utapanda punda au utapanda nini Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba tunaomba lami toa fedha Wizara ya Fedha toeni fedha ili tujenge barabara ya lami Barabara yetu ya Ziba - Puge hii barabara tumeisema miaka yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii barabara tunaisema kila siku tunaomba na sisi tupewe fedha tujenge barabara ya lami kero yangu kubwa ni hiyo Mheshimiwa Waziri kwenye hii bajeti mmetupa lakini tunaomba utekelezaji fedha zitoke mwaka jana mmetuandikia mnatupa mwaka juzi mmeandika mnatupa sasa mwaka huu mzitoe hizo hela ili tuende kwenye utekelezaji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya ahsante Mheshimiwa.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Gulamali wewe na Waziri wote si mko mtaa mmoja kule? Si mzungumze kule? *(Makofi)*

Wageni waliopo bungeni wageni 16 wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa Naibu Waziri wa Madini, Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Longido Mkoa wa Arusha wakiongozwa na Mwenyekiti wao Papa Nakuta, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe kikao cha saa saba mchana Msekwa, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 6.45 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 26 Juni, 2024, Saa Tatu Asubuhi)*